# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR NAM. 1 YA 2012 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU MAELEZO


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Matumizi.

3. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA MAMLAKA

4. Kuanzishwa kwa Mamlaka.

5. Kazi za Mamlaka.

### SEHEMU YA TATU
### USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

6. Uteuzi na sifa za Mkurugenzi Mkuu.

7. Kazi na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu.

8. Muda wa Mkurugenzi Mkuu.

9. Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu.

10. Kiapo cha Mkurugenzi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu.

11. Kuanzishwa kwa Ofisi za Mikoa na Wilaya.

12. Idara, vitengo, divisheni na sehemu za Mamlaka.

13. Wafanyakazi

14.` Kiapo.

15. Usiri.

16. Kutangaza mali na madeni.

## SEHEMU YA NNE
## UCHUNGUZI

17. Uwezo maalum wa uchunguzi.

18. Mashirikiano katika uchunguzi.

19 Uwezo wa Mamlaka kukusanya taarifa za kiintelijensia.

20. Mchunguzi na msaidizi Mchunguzi.

21. Uwezo wa Mamlaka kumhoji mtu.

22. Kitambulisho cha Mchunguzi.

23. Lalamiko lisilochunguzwa.

24. Maelezo ya mali za mtuhumiwa.

25. Masharti ya kutoa taarifa za mali za mshirika wa mtuhumiwa.

26. Kuondoshwa kwa wajibu wa kuficha siri.

27. Utoaji wa kumbukumbu na mali.

28. Kufanya upekuzi wa majengo.

29. Uhalali wa ushahidi kwa vitu vilivyowasilishwa au vilivyopatikanwa.

30. Kusalimisha hati za kusafiria.

31. Kumkamata mtu.

32. Utoaji wa taarifa ambazo zinaweza kuharibu uchunguzi.

33. Kujifananisha.

34. Ripoti ya uchunguzi.

35. Kazi kufanywa kwa nia njema.

## SEHEMU YA TANO
## MAKOSA YA RUSHWA

36. Rushwa.

37. Rushwa ya wakala.

38. Rushwa inayofanywa na Afisa wa Umma.

39. Rushwa kwa Afisa wa Umma.

40. Kuomba au kupokea faida kinyume na sheria kwa mtu anayefanya au kutekeleza maamuzi ya Mahakama.

41. Rushwa katika minada.

42. Ushawishi wa siri katika kutoa ushauri.

43. Rushwa kwa ajili ya kutoa msaada kuhusu mkataba.

44. Kumdanganya mkuu.

45. Mgongano wa maslahi.

46. Faida isiyoruhusiwa kwa wadhamini kwa kuteuliwa.

47. Rushwa ya zabuni.

48. Matumizi mabaya ya wadhifa.

49. Uhaulishaji wa mapato ya rushwa.

50. Rushwa katika uchaguzi.

51. Rushwa ya Afisa wa kigeni.

52. Kushawishi au kufanya rushwa ya ngono.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA YA UHUJUMU UCHUMI

53. Matumizi mabaya ya mali ya Umma.

54. Matumizi mabaya ya mali na mapato.

55. Matumizi mabaya ya mali.

56. Kukwepa kodi.

57. Hasara inayotokana na uzembe.

58. Magendo.

59. Kuhodhi.

60. Kufanya jambo kinyume na ushindani wa soko.

61. Matumizi mabaya ya taarifa rasmi.

62. Utakatishaji wa fedha haramu.

63. Usafirishaji wa dawa za kulevya.

64. Bidhaa, fedha au huduma bandia.

65. Biashara ya fedha kinyume na sheria.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

66. Kumzuia Mtumishi.

67. Adhabu ya jumla.

68. Faini ya ziada ya lazima.

## SEHEMU YA NANE
## FIDIA YA UREJESHAJI WA FAIDA ISIYOFAA

69. Wajibu wa kulipa fidia.

70. Wajibu kwa manufaa yasiyofaa.

71. Wajibu mbali mbali.

72. Amri ya fidia baada ya kutiwa hatiani.

73. Kutaifisha mali ambayo haina maelezo.

74. Utaifishaji wa mali.

75. Amri ya kuzuia mali inayotuhumiwa.

76. Maombi kwa amri ya uzuiaji.

77. Amri ya zuio.

78. Ukamataji wa mali inayohamishika.

79. Urejeshaji wa fedha na mali nyenginezo.

80. Mashauri yanayotokana na utaifishaji.

81. Malipo mbadala wa kufilisi.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI KUHUSU USHAHIDI

82. Mali isiyo na maelezo kama kuwa ushahidi wa nyongeza.

83. Hati ya kuonyesha thamani ya mali.

84. Kanuni na taratibu kuhusiana na mshirika wa kosa.

85. Hati inayoonesha ofisi.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI YA FEDHA

86. Fedha na rasilimali za Mamlaka.

87. Bajeti.

88. Hesabu na ukaguzi.

89. Kufungua akaunti ya benki.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MASHARTI MENGINEYO

90. Ripoti ya mwaka.

91. Ushughulikiaji wa tuhuma dhidi ya mfanyakazi.

92. Kumsaidia mtu kutenda kosa.

93. Ushughulikiaji wa mali iliyotelekezwa.

94. Kusimamishwa kazi kwa kushtakiwa kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi.

95. Mfanyakazi kuchukuliwa kama Afisa wa Chuo cha Mafunzo.

96. Kutokuwa na sifa kwa mtu aliyetiwa hatiani.

97. Kutangazwa kwa mtu aliyepatikana na hatia ya rushwa au uhujumu uchumi.

98. Kulindwa kwa mtoa taarifa.

99. Kulindwa kwa shahidi.

100. Wajibu wa kuripoti faida.

101. Kinga kwa mfanyakazi.

102. Mila sio utetezi.

103. Kutowezekana au kutokuwa na nia sio utetezi.

104. Mashirikiano na mamlaka nyengine.

105. Mashirikiano na sekta binafsi.

106. Msaada wa nje.

107. Kubadilishana wahalifu.

108. Kitendo kilichofanywa nje ya Zanzibar.

109. Ufunguaji wa mashtaka.

110. Mahakama za usikilizaji wa mashauri.

111. Kanuni.

112. Miongozo.

113. Kufuta na kubakiza.

**JADWELI**

**SHERIA NAM. 5 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

24 JULAI, **2023**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR NAM. 1 YA 2012 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kwa tarehe itakayotangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika katika mambo yote yanayohusiana na usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka na mambo yote yanayohusiana na kuzuia na kupambana na rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Afisa" maana yake ni mtu aliyeajiriwa au aliyeteuliwa kushika nafasi katika taasisi ya umma au binafsi;

"amri ya zuio" maana yake ni amri iliyotolewa na Mahakama kuzuia mali maalum ya mtuhumiwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"data" maana yake ni taarifa zilizorikodiwa au zilizohifadhiwa kwa namna ambayo zinaweza kuchakatwa kwa kutumia kifaa kinachofanya kazi wenyewe kwa kufuata maelekezo kilichopewa kwa madhumuni hayo;

"faida" maana yake ni zawadi yoyote, mkopo, ada, marejesho, uteuzi, huduma, upendeleo, zuio la kutekeleza jambo halali, ahadi, fursa au malipo mengine;

"Kamanda wa Mamlaka wa Mkoa" maana yake ni mfanyakazi aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu chini ya masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria hii;

"Kamanda wa Mamlaka wa Wilaya" maana yake ni mfanyakazi aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu chini ya masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria hii;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"kitendo cha rushwa" maana yake ni kitendo ambacho:

(a) kinapelekea makosa ya rushwa au uhujumu uchumi; au

(b) kilifanywa kabla ya Sheria hii kuanza kutumika na ambacho kwa wakati huo kilikuwa ni kosa la rushwa au uhujumu uchumi;

"Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu (FIU)" maana yake ni Kitengo kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009;

"mali zisizoelezeka" maana yake ni mali:

(a) zilizopatikana katika au karibu na muda ambao mtu anadaiwa kutenda kosa la rushwa au uhujumu uchumi; au

(b) ambazo thamani ya mali hizo hazilingani na vyanzo vya kipato vinavyojulikana vya mtu huyo katika au karibu na muda huo ambapo hakuna maelezo ya kuridhisha kuhusiana na upatikanaji wa mali hizo;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Mchunguzi Msaidizi" maana yake ni mfanyakazi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu chini ya masharti ya kifungu cha 20 cha Sheria hii kumsaidia Mchunguzi;

"mtoa huduma za mawasiliano" maana yake ni mtu anayetoa huduma za posta, taarifa au mawasiliano ikijumuisha mawasiliano ya simu, vyombo vya habari, tovuti, blogu, huduma za mitandao, huduma za intaneti na mtaalam ambaye ametangazwa na Mkurugenzi Mkuu;

"Mchunguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu chini ya masharti ya kifungu cha 20 cha Sheria hii kufanya uchunguzi;

"Mkuu" inajumuisha:

(a) mnufaika;

(b) mtu ambaye wakala anafanya kazi kwa niaba yake; na

(c) muajiri.

"Mfanyakazi" maana yake ni mtumishi au afisa yeyote wa Mamlaka, ikijumuisha Mkurugenzi Mkuu, Naibu Mkurugenzi Mkuu na kila mtu aliyeajiriwa na au anatoa huduma za Mamlaka;

"Naibu Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Naibu Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"rushwa" inajumuisha makosa yote yaliyoainishwa chini ya Sehemu ya Tano ya Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Shirika la umma" maana yake ni shirika lolote lililoanzishwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Nam. 6 ya 2021 au chini ya sheria nyengine yoyote na ambapo Serikali au wakala wake inamiliki hisa nyingi zaidi au hisa zote katika Shirika hilo;

"Taasisi ya umma" maana yake ni taasisi yoyote au chombo kinachofanya kazi ya au kwa niaba ya Serikali;

"Taasisi " maana yake ni taasisi au afisi yoyote ya umma au binafsi ambayo inatoa ajira chini ya mkataba wa ajira, mkataba wa huduma au vyenginevyo, ajira ya muda au ya kudumu au kwa malipo au bila ya malipo;

"Uhujumu Uchumi" maana yake ni makosa yaliyoainishwa chini ya Sehemu ya Sita ya Sheria hii;

"wakala" inajumuisha:

(a) mtu aliyeajiriwa ikiwa yupo katika mkataba wa ajira, mkataba wa huduma au vyenginevyo ajira ya kudumu au ya muda au kwa malipo au bila ya malipo;

(b) mdhamini;

(c) msimamizi au kiongozi wa mali za marehemu; au

(d) mfanyakazi wa umma.

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA MAMLAKA

Kuanzishwa kwa Mamlaka.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ambayo kwa jina fupi itakuwa "ZAECA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye urithi wa kuendelea, muhuri na kwa jina lake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kushikilia na kuondoa mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika; na

(c) kutekeleza jambo jengine lolote ambalo kisheria linaweza kutekelezwa na chombo kinachojitegemea.

Kazi za Mamlaka.

**5.**-(1) Kazi za Mamlaka ikiwa na hadhi ya uaskari, zitakuwa ni:

(a) kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote kuhusu kitendo cha rushwa katika taasisi yoyote ya umma au binafsi;

(b) kuchunguza jambo lolote ambalo, kwa maoni ya Mamlaka, linaibua dhana kuwa moja kati ya mambo yafuatayo yametokea au yanaweza kutokea:

(i) kitendo kinachopelekea kosa la rushwa au uhujumu uchumi; na

(ii) kitendo kinachoweza kuruhusu, kushawishi au kusababisha kuwepo kwa kitendo cha kosa la rushwa au uhujumu uchumi;

(c) kuchunguza vitendo vya mtu yeyote ambavyo, kwa maoni ya Mamlaka, vinapelekea kuwepo kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi au kosa jengine chini ya Sheria hii;

(d) kuisaidia taasisi yoyote ya Serikali inayosimamia sheria katika kuchunguza kosa la rushwa au uhujumu uchumi;

(e) kwa maombi ya mtu yeyote, kushauri na kusaidia juu ya njia ambazo zitamuwezesha mtu huyo kuzuia kitendo cha rushwa;

(f) kuchunguza mienendo au taratibu katika taasisi za umma au binafsi ili kuwezesha kubaini kitendo cha rushwa na kuona namna ya kuimarisha mienendo na taratibu za utendaji kazi ambazo, kwa maoni ya Mamlaka, zitapelekea kuwepo kwa kitendo cha rushwa;

(g) kumuelekeza Afisa Mtendaji Mkuu yeyote wa taasisi juu ya mabadiliko ya matendo au taratibu zinazoendana na utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi katika taasisi hizo ambapo Mkurugenzi Mkuu ataona ni muhimu kupunguza uwezekano wa kutokea kitendo cha rushwa;

(h) kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kanuni za maadili, madhara ya rushwa na uhujumu uchumi na kuitaka jamii kuisaidia Mamlaka katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi na kwa msingi huo, Mamlaka:

(i) itabuni na kuchapisha aina yoyote ya machapisho yanayofaa kwa dhamira na madhumuni yake;

(ii) itaanzisha au kufanya utafiti au upembuzi wowote;

(iii) itaandaa makongamano, mikusanyiko au mikutano yoyote na kushiriki katika kongamano lolote linaloandaliwa na taasisi nyengine; na

(iv) itabuni na kutekeleza programu za kuelimisha umma kuhusu masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kupitia vyombo vya habari.

(i) kuchunguza kiwango cha uwajibikaji kwa upotevu au uharibifu wa mali yoyote ya umma na kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu, kufungua mashauri ya madai dhidi ya mtu yeyote ili kurejesha mali hiyo au fidia;

(j) kurejesha mali iliyopotea au iliyoharibiwa au kutekeleza amri ya fidia hata ikiwa mali iliyopotea au iliyoharibiwa ipo nje ya Zanzibar au mali ambayo inaweza kutumika kutekeleza amri ipo nje ya Zanzibar;

(k) kusimamia mikataba na miradi ambayo Serikali inanufaika moja kwa moja au vyenginevyo kabla ya kufungwa kwa mikataba na wakati wa utekelezaji wake; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote iliyopewa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

(2) Afisa Mtendaji Mkuu wa taasisi atafuata maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1)(g) cha kifungu hiki.

(3) Endapo taasisi itaona kwamba hailazimiki kufuata maelekezo yaliyotolewa katika kifungu kidogo cha (1)(g) cha kifungu hiki, itatoa maelezo, kwa maandishi kwa Mamlaka si zaidi ya siku kumi na nne kuanzia siku ya maelekezo kuwa taasisi hiyo hailazimiki kufuata maelekezo hayo.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, Mamlaka inaweza kumpangia kazi mfanyakazi au mchunguzi katika taasisi yoyote kama Mkurugenzi Mkuu atakavyoona inafaa.

(5) Mtu ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

Uteuzi na sifa za Mkurugenzi Mkuu.

**6.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya sheria au fani nyengine yoyote kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka saba katika fani ya sheria, uchunguzi wa makosa ya jinai, uendeshaji mashtaka, utoaji wa haki, uongozi au utawala;

(d) ana uadilifu wa hali ya juu; na

(e) hajawahi kutiwa hatiani katika mahakama yoyote kwa kosa la rushwa, uhujumu uchumi au kosa jengine linalohusiana na fedha.

Kazi na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu.

**7.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atatekeleza kazi za kila siku za Mamlaka.

(2) Katika kutekeleza kazi za Mamlaka chini ya Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu atakuwa na uwezo wa:

(a) kumuidhinisha mfanyakazi yeyote kutumia uwezo au kutekeleza jukumu lolote ambalo Mkurugenzi Mkuu kwa Sheria hii au sheria yoyote ametakiwa kufanya au kutekeleza;

(b) kumuidhinisha mfanyakazi yeyote kufanya uchunguzi au upelelezi juu ya kosa lolote linalotuhumiwa chini ya Sheria hii;

(c) kupanga na kupandisha vyeo kwa wafanyakazi kwa kuzingatia muundo wa utumishi wa Mamlaka;

(d) kumtaka mtu yeyote, kwa maandishi, kutoa kitabu, kumbukumbu, marejesho, ripoti, kitabu cha benki, au taarifa za akaunti ya benki, taarifa zilizohifadhiwa katika njia za kielektroniki katika kompyuta au vyenginevyo na nyaraka nyengine zozote zinazotuhumiwa kuhusika katika vitendo vya rushwa au uhujumu uchumi ndani ya muda maalum;

(e) kumtaka mtu yeyote ndani ya muda ulioainishwa kufika katika Mamlaka na kujibu swali lolote ambalo Mkurugenzi Mkuu ataona ni muhimu kuhusiana na uchunguzi wowote ambao anaufanya chini ya Sheria hii;

(f) kumzuia mtuhumiwa endapo kutakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba ametenda kosa chini ya Sheria hii;

(g) kusimamisha kwa muda matumizi ya akaunti **yoyote** ya benki kupisha uchunguzi;

(h) kuitaarifu taasisi yoyote kwa maandishi juu ya afisa ambaye yupo chini ya uchunguzi wa kosa lolote chini ya Sheria hii, kwamba kwa maoni yake afisa huyo ametenda kosa la kinidhamu; na

(i) kuteua maeneo ya ofisi za Mamlaka na kuyatangaza kuwa maeneo maalum yaliyotengwa na kuzuiwa kutoingiwa bila ya ruhusa maalumu.

(3) Mtu atakayeshindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (2)(d), (e) na (g) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

(4) Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake chini ya kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu hatokuwa chini ya maelekezo au udhibiti wa mtu au mamlaka nyengine yoyote.

Muda Mkurugenzi Mkuu.

**8.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atashika nafasi yake muda wote na hatojishughulisha na kazi nyengine yoyote ambayo atakuwa analipwa mshahara kwa namna yoyote.

(2) Mkurugenzi Mkuu hatoondolewa katika wadhifa wake isipokuwa kwa sababu na kwa mujibu wa utaratibu wa kumuondoa kazini Jaji wa Mahakama Kuu ulioainishwa katika masharti ya Katiba.

Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu.

**9.**-(1) Kutakuwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo anazo sifa kama za Mkurugenzi Mkuu.

(3) Naibu Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Masuuli wa Mamlaka na Msaidizi Mkuu wa Mkurugenzi Mkuu na atafanya kazi na majukumu ya Mamlaka chini ya maelekezo ya Mkurugenzi Mkuu.

(4) Endapo Mkurugenzi Mkuu hayupo, Naibu Mkurugenzi Mkuu atafanya kazi na majukumu ya Mkurugenzi Mkuu.

Kiapo cha Mkurugenzi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu.

**10**. Mkurugenzi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu, kabla ya kutekeleza majukumu yao, wataapa mbele ya Rais kwa mujibu wa masharti ya sheria zinayohusika.

Kuanzishwa kwa ofisi za Mikoa na Wilaya.

**11.**-(1) Kutakuwa na Ofisi za Mamlaka za Mikoa na Wilaya ambazo zitaongozwa na Makamanda wa Mikoa na Wilaya.

(2) Hadhi, sifa na mambo mengine yanayowahusu Makamanda wa Mamlaka wa Mikoa na Wilaya yataainishwa katika Kanuni.

Idara, vitengo, divisheni na sehemu za Mamlaka.

**12.**-(1) Mamlaka inaweza kuanzisha idara, vitengo, divisheni, sehemu au ofisi nyengine kama itavyoonekana inafaa kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake.

(2) Wakurugenzi, Makamanda wa Mamlaka wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa vitengo, divisheni, sehemu au maofisa wengine wa Mamlaka watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi.

**13.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, isipokuwa katika hali yoyote ambayo kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa wafanyakazi bora, Mamlaka, inaweza kuajiri au kuteua wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuzingatia vigezo na masharti kama Mkurugenzi Mkuu atakavyoamua.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake, Mamlaka inaweza kuajiri mtaalamu elekezi, mtaalamu au mchunguzi wa kujitegemea kama itakavyohitajika.

(3) Kwa lengo la kulinda uhuru na uadilifu wa Mamlaka, mfanyakazi isipokuwa kwa uteuzi wa Rais, hatoweza kuhamishwa kwenda au kutoka Mamlaka bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu.

(4) Mkurugenzi Mkuu atatoa kitambulisho kwa mfanyakazi kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Kiapo.

**14.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 10 cha Sheria hii, kila mfanyakazi, kabla ya kuanza majukumu yake kwenye Mamlaka, atakula kiapo kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Usiri.

**15.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 10 cha Sheria hii, kila mfanyakazi atakula kiapo cha kutunza siri kwa namna na taratibu zilizoainishwa chini ya kanuni.

(2) Mfanyakazi, hatoruhusiwa isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote:

(a) kufichua taarifa yoyote aliyoipata wakati wa kutekeleza mamlaka yake au katika kutekeleza majukumu aliyopewa chini ya Sheria hii; na

(b) kufichua chanzo cha taarifa au utambulisho wa mtoa taarifa, mtayarishaji au mwandishi yeyote wa taarifa zilizopokelewa na Mamlaka,

(3) Mfanyakazi ataendeleza usiri na unyeti wa jambo lolote, nyaraka, ripoti na taarifa nyengine zinazohusiana na usimamizi wa Sheria hii ambazo amezijua, amezimiliki au zipo chini ya udhibiti wake.

(4) Mfanyakazi aliyeidhinishwa kupokea taarifa atazichukulia taarifa hizo kuwa za usiri wa hali ya juu na hatozitoa taarifa hizo kwa njia yoyote ile kwa mtu mwengine isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi Mkuu.

(5) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) vya kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu anaweza kutoa, kwa madhumuni ya kuchapisha kwa vyombo vya habari, taarifa ambayo ataona ina umuhimu katika maslahi ya umma.

(6) Kwa madhumuni ya uchunguzi kuhusiana na kosa lililotendeka Zanzibar chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusiana na udhibiti wa fedha haramu, Mkurugenzi Mkuu, kwa makubaliano na taasisi inayohusika, anaweza kutoa taarifa hizo akiona kwamba kufanya hivyo kutasaidia uchunguzi wa kosa la utakatishaji wa fedha haramu au kosa jengine lolote.

(7) Mfanyakazi ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki bila sababu ya kisheria, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atafungwa kifungo cha muda usiopungua miaka mitatu na usiozidi miaka mitano.

Kutangaza mali na madeni.

**16.**-(1) Mfanyakazi, isipokuwa aliyetakiwa kutangaza mali chini ya masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015 kwa kadri ya uelewa wake, ataweka wazi taarifa sahihi aliyotakiwa kuiweka wazi, sio zaidi ya siku thelathini tokea tarehe ya kuteuliwa kwake.

(2) Mfanyakazi atawasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu taarifa sahihi ya mwaka ndani au kabla ya mwezi wa Novemba wa kila mwaka kwa kujaza na kuwasilisha fomu kama ilivyoainishwa chini ya kanuni.

(3) Mfanyakazi ambayeataficha taarifa, atatoa taarifa za uongo au maelezo ya kupotosha, hatoweka wazi taarifa sahihi au hatofuata masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "taarifa sahihi" maana yake ni taarifa kuhusiana na mali na utajiri mwengine chini ya umiliki au aina nyengine yoyote ya udhibiti wa mfanyakazi na mwenza wake.

## SEHEMU YA NNE
## UCHUNGUZI

Uwezo maalum wa uchunguzi.

**17.**-(1) Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu, anaweza:

(a) kuamuru mtu yeyote kufika mbele ya Mkurugenzi Mkuu kwa madhumuni ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote ambalo kwa maoni ya Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi, litasaidia katika uchunguzi wa kosa linalodaiwa;

(b) kuamuru mtu yeyote kutoa kitabu chochote, nyaraka, nakala yoyote iliyothibitishwa au andiko lolote ambalo linaweza kusaidia katika uchunguzi wa kosa linalodaiwa; au

(c) kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mtu yeyote kutoa maelezo kwa kiapo au uthibitisho unaoelezea taarifa hiyo ambayo inaweza kusaidia katika uchunguzi wa kosa linalodaiwa.

(2) Mtu ambaye, wakati wa uchunguzi wa kosa linalodaiwa chini ya Sheria hii, huku akijua:

(a) anatoa au anasababisha kutolewa ripoti au taarifa za uongo kuhusiana na kufanyika kwa kosa linalodaiwa kwa Mchunguzi yoyote;

(b) anampotosha Mchunguzi; au

(c) anashindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki,

ametenda kosa.

Mashirikiano katika uchunguzi.

**18.**-(1) Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi, wakati wa kufanya uchunguzi, anaweza kufanya kazi kwa kushirikiana na mtu yeyote anayemuhisi ni muhimu katika kumshirikisha huko, na itakuwa ni jukumu la mtu huyo kutoa mashirikiano hayo.

(2) Mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Uwezo wa Mamlaka kukusanya taarifa za kiintelijensia.

**19.**-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa madhumuni ya kuzuia au kubaini kosa la rushwa au la uhujumu uchumi au kwa madhumuni ya uendeshaji mashtaka dhidi ya mtuhumiwa chini ya Sheria hii, kutoa maelekezo kama ataona inafaa, kwa:

(a) mtoa huduma za mawasiliano kwa ujumla;

(b) mtoa huduma za mawasiliano kwa maelezo maalum; au

(c) mtoa huduma za mawasiliano yeyote.

(2) Maelekezo chini ya kifungu hiki yataeleza ukomo wa muda ambao mtoa huduma za mawasiliano anaweza kuhitajika kuzihifadhi data za mawasiliano.

(3) Endapo mtoa huduma za mawasiliano atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Mahakama inaweza, kwa ombi la Mkurugenzi Mkuu, ikamuamuru mtoa huduma za mawasiliano kufanyia kazi maelekezo hayo.

Mchunguzi na msaidizi Mchunguzi.

**20.**-(1) Kutakuwa na Mchunguzi na Msaidizi Mchunguzi ambao watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu miongoni mwa wafanyakazi, baada ya kukamilisha mafunzo ya awali ya uchunguzi yanayotolewa na Mamlaka.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu anaweza kuteua wachunguzi wa muda kwa muda mahsusi na kazi maalum.

(3) Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi anaweza kufanya uchunguzi na:

(a) atawajibika kwa uchunguzi wowote atakaotakiwa na Mamlaka kuufanya unaohusisha rushwa na uhujumu uchumi;

(b) atawajibika kwa uchunguzi wowote unaohusiana na utakatishaji fedha ambao Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu (FIU) kitauwasilisha kwa Mamlaka;

(c) kwa kuzingatia masharti yoyote yaliyowekwa chini ya Sheria hii, miongozo iliyotolewa chini ya Sheria hii na kanuni, atatekeleza uwezo wa Mamlaka kama ulivyokasimiwa kwake na Mamlaka kuhusiana na makosa ya rushwa na uhujumu uchumi;

(d)ataripoti kwa Mamlaka juu ya uchunguzi wowote aliotakiwa kuufanya; na

(e) atafuata maelekezo yote ya Mamlaka yanayohusiana na kazi zake.

(4) Kwa madhumuni ya uchunguzi, Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi, mbali ya uwezo aliokuwa nao chini ya Sheria hii, atakuwa na uwezo, fursa na kinga za Afisa wa Polisi wa cheo cha au zaidi ya Mrakibu Msaidizi wa Polisi kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi [Sura 322], Sheria ya Kamisheni ya Jeshi la Polisi na Magereza [Sura 241] na Kanuni zake, zenye umuhimu kwa ajili ya kuzuia, kupambana na kuchunguza kosa.

(5) Kwa mujibu wa sheria zinazosimamia taratibu za kupata, kumiliki na kutumia silaha za moto na risasi, katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii, Mamlaka itakuwa na uwezo na haki ya kupata, kumiliki na kutumia silaha za moto na risasi.

Uwezo wa Mamlaka kumhoji mtu.

**21.**-(1) Endapo Mamlaka imeamua kuendelea na uchunguzi wowote inaweza, kwa kuzingatia kanuni au muongozo, kuamuru mtu:

(a) kufika mbele ya Mamlaka kwa lengo la kuhojiwa kwa njia ya ana kwa ana kuhusiana na jambo lolote chini ya Sheria hii;

(b) kuwasilisha mbele ya Mamlaka kitabu chochote, nyaraka, kumbukumbu au andiko;

(c) kusababisha taarifa zilizohifadhiwa katika kompyuta, diski, kaseti au katika mkanda wa filamu au zilizohifadhiwa na kifaa chochote cha kielektroniki au mashine kuwasilishwa katika mfumo ambao kinaweza kuchukulika, kuonekana na kufahamika; na

(d) kuwasilisha kwa maandishi maelezo yaliyofanywa kwa kiapo au uthibithisho, yenye taarifa zote ambazo zitahitajika chini ya notisi.

(2) Mtu ambaye amepewa amri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) atatii amri hiyo;

(b) atafika mbele ya Mkurugenzi Mkuu kwa mujibu wa masharti ya amri;

(c) ataendelea kufika katika siku nyengine kama atakavyoelekezwa na Mkurugenzi Mkuu mpaka pale mahojiano yatakapokamilika; na

(d) kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, atajibu maswali na kuwasilisha taarifa zote, nyaraka, kumbukumbu

au maelezo ikijumuisha nakala za nyaraka zilizothibitishwa kama alivyoamriwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Endapo Mkurugenzi Mkuu atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba kitabu chochote, nyaraka, kumbukumbu au andiko lililowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (2)(d) cha kifungu hiki, linaweza kuisaidia Mamlaka katika ushahidi kwa uchunguzi unaofanywa, anaweza:

(a) kuzuia kitabu, nyaraka, kumbukumbu au andiko, endapo hakuna sababu za msingi za kuhitajika kwa madhumuni ya kutekeleza jukumu lolote chini ya sheria yoyote, mpaka pale itakapowasilishwa mahakamani au mapema zaidi itakapohitajika; au

(b) kutayarisha nakala zilizothibitishwa au kuchukuwa kumbukumbu kutoka kwenye kitabu, nyaraka au andiko.

(4) Mtu ambaye, baada ya kupewa amri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) atashindwa, bila ya sababu za msingi kufuata sharti lolote la amri;

(b) ataficha, ataharibu, atabadilisha, ataingilia, atahamisha kutoka eneo inapowekwa kikawaida au vyenginevyo atapoteza kitabu, nyaraka, kumbukumbu au andiko lililotajwa katika amri hiyo,

ametenda kosa na, akipatikana na hatia, atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano.

Kitambulisho cha Mchunguzi.

**22.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Miongozo, atatoa kitambulisho kwa mfanyakazi aliyeteuliwa kuwa mchunguzi ambacho kitatumika kama ushahidi kuwa mfanyakazi huyo ni mchunguzi.

(2) Kitambulisho kilichotolewa chini ya masharti ya kifungu hiki, kitasainiwa na Mkurugenzi Mkuu na mwenye kitambulisho hicho.

Lalamiko lisilochunguzwa.

**23.** Endapo Mamlaka imepokea lalamiko kuhusiana na kitendo cha rushwa au uhujumu uchumi kwa mtu yeyote na ikakataa kuchunguza au ikaacha kufanya uchunguzi, Mkurugenzi Mkuu atamtaarifu kwa maandishi mlalamikaji juu ya uamuzi wake huo na sababu za kuchukua uamuzi huo.

Maelezo ya mali za mtuhumiwa.

**24.**-(1) Mamlaka inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mtu ambaye kuna sababu za kutuhumiwa na kosa la rushwa au uhujumu uchumi, kuwasilisha maelezo kwa maandishi ndani ya muda unaofaa uliotajwa katika taarifa, ya:

(a) kuhesabu mali za mtuhumiwa na wakati ambao mali hiyo imepatikanwa; na

(b) kuelezea kuhusu mali yoyote ambayo imepatikana kwa wakati huo au karibu na kipindi kinachotuhumiwa kufanyika kosa la rushwa au uhujumu uchumi, ikiwa mali hiyo imepatikana kwa kununuliwa, zawadi, urithi au kwa njia nyengine, na kiwango cha gharama, kama ipo ya kupatikana kwa mali hiyo.

(2) Mtu ambaye ataacha au atashindwa kufuata masharti yaliyoainishwa chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa.

Masharti ya kutoa taarifa za mali za mshirika wa mtuhumiwa.

**25.**-(1) Mamlaka inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumuagiza mshirika wa mtuhumiwa, ndani ya muda ulioelezwa katika taarifa hiyo kuwasilisha maelezo ya maandishi ya mali zake.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, neno:

(a) "mshirika wa mtuhumiwa" maana yake ni mtu, ama ametuhumiwa au hajatuhumiwa kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi, ambaye mchunguzi ana sababu za kuamini kwamba anajihusisha na mali za mtuhumiwa; na

(b) "mali za mtuhumiwa" maana yake ni mali za mtu anayetuhumiwa kwa kosa la rushwa au la uhujumu uchumi.

(3) Mamlaka inaweza, kwa taarifa ya maandishi na ndani ya muda unaofaa uliotajwa katika taarifa, kumtaka mtu yeyote kuwasilisha taarifa au nyaraka zozote zilizokuwepo katika udhibiti wake ambazo zinahusishwa na mtuhumiwa wa rushwa au uhujumu uchumi.

(4) Mtu ambaye atakiuka masharti ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) vya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa.

(5) Mtu ambaye, kwa kujua atajihusisha na mali ambazo anaamini au ana sababu za kuamini kwamba zimepatikana kwa matokeo ya kitendo cha rushwa, ametenda kosa, endapo mtu huyo:

(a) anashikilia, anapokea, anaficha, anatumia au anawezesha kutumika kwa mali hiyo; au

(b) anaingia kwenye miamala au anawezesha kuingiwa kwa miamala kuhusiana na mali hiyo.

Kuondoshwa kwa wajibu wa kuficha siri.

**26.** Kwa jambo lolote linalohusiana na miamala ya fedha au kodi, masharti ya Sheria hii yatatekelezwa bila ya kujali wajibu wowote wa kutunza siri au vizuizi vyengine juu ya utoaji wa taarifa au kuwasilisha nyaraka, yaliyoainishwa katika sheria yoyote au vyenginevyo.

Utoaji wa kumbukumbu na mali.

**27.**-(1) Mamlaka inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mtu ikiwa anatuhumiwa au hatuhumiwi kufanya kosa la rushwa au uhujumu uchumi, kutoa kumbukumbu mahsusi alizonazo ambazo zinahitajika katika uchunguzi na kumtaka mtu huyo au mtu mwengine yeyote kutoa maelezo au taarifa anazozifahamu kuhusiana na kumbukumbu ikiwa kumbukumbu hizo zimetolewa na mtu huyo au vyenginevyo.

(2) Sharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, linaweza kujumuisha sharti la kumtaka mtu huyo kufika yeye binafsi mbele ya Mamlaka ili kutoa maelezo na taarifa.

(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote chini ya Sheria hii, Mamlaka inaweza kutoa nakala ya au kuchukua kutoka katika kumbukumbu yoyote iliyowasilishwa chini ya masharti ya kifungu hiki.

(4) Sharti chini ya kifungu hiki likihusisha kumbukumbu zilizohifadhiwa kwa njia ya kielektroniki ni sharti la kuwasilisha kumbukumbu kwa njia ya nakala ngumu na endapo kwa mahsusi atatakiwa kuwasilisha kwa njia ya kielektroniki, atapaswa kuwasilisha kwa njia ya kieletroniki.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kumbukumbu" inajumuisha vitabu, marejesho, hesabu za benki au hesabu nyengine, ripoti, nyaraka za kisheria au za kibiashara na mawasiliano mengine isipokuwa mawasiliano binafsi.

(6) Mamlaka inaweza, kwa taarifa ya maandishi na kwa muda mahsusi uliotajwa katika taarifa hiyo, kumtaka mtu kuwasilisha mali yoyote ya mtu aliyetuhumiwa kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi ambaye ipo chini ya dhamana yake, kwa ajili ya uchunguzi.

(7) Mtu ambaye atakataa au atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa.

Kufanya upekuzi wa majengo.

**28.**-(1) Mkurugenzi Mkuu au mtu mwengine yeyote aliyemuidhinisha anaweza, kwa hati au bila ya hati ya upekuzi, kuingia katika jengo lolote na kufanya upekuzi wa kumbukumbu yoyote, mali au kitu chengine ambacho kuna sababu ya kushukiwa kuwa kimo ndani ya jengo hilo na ambacho hakikuwasilishwa na mtu kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti chini ya kifungu cha 20(4) cha Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi anaweza, muda wowote, kuingia na kufanya upekuzi katika jengo lolote ambalo ana sababu ya kuamini kuwa ushahidi wa kosa utapatikana au kosa linatendeka au litatendeka.

(3) Mkurugenzi Mkuu au Mchunguzi atafuata taratibu za upekuzi zilizoainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam. 7 ya 2018.

(4) Mchunguzi ambaye, bila ya sababu za msingi, ataamrisha, ataidhinisha au atafanya upekuzi wa mtu, sehemu, jengo au chombo atakuwa ametenda kosa.

Uhalali wa ushahidi kwa vitu vilivyowasilishwa au kupatikanwa.

**29.**-(1) Kitu chochote kitakachowasilishwa na mtu kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au kilichopatikana katika jengo wakati wa upekuzi au wakati wa kumkamata mtuhumiwa wa kosa la rushwa au uhujumu uchumi, Mamlaka inaweza kukichukua na kukihifadhi kwa muda unaofaa kwa madhumuni ya uchunguzi na kitakubalika kama ushahidi katika uendeshaji wa mashtaka ya mtu yeyote, ikijumuisha mtu aliyekiwasilisha au aliyekamatwa nacho.

(2) Baada ya mashauri kukamilika chini ya Sheria hii, hakutokuwa na shauri lolote kisheria litakalofunguliwa Mahakamani dhidi ya Mamlaka kwa jambo lolote lililotokea kwa vitu vilivyowasilishwa au vilivyopatikana katika upekuzi wa eneo au kwa kumkamata mtuhumiwa wa kosa la rushwa au uhujumu uchumi.

Kusalimisha hati za kusafiria.

**30.**-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kumtaka mtu yeyote kusalimisha hati zake za kusafiria kwa Mamlaka ikiwa mtu huyo kuna sababu za kumshuku kuwa ametenda kosa la rushwa au uhujumu uchumi au kuna uchunguzi unaoendelea juu ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi.

(2) Endapo mtu atasalimisha hati zake za kusafiria kwa mujibu wa amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka:

(a) itarudisha hati hizo baada ya kukamilisha uchunguzi wa kosa la rushwa au uhujumu uchumi na ikiwa hakuna mashtaka ya jinai yaliyofunguliwa; au

(b) ikiwa uchunguzi haujakamilika:

(i) inaweza kurudisha hati za kusafiria kwa masharti au bila masharti; au

(ii) itarudisha hati hizo sio zaidi ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kusalimisha.

(3) Mtu ambaye hati zake za kusafiria zimezuiliwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza kuiomba Mahakama kutoa amri kwa Mamlaka ya kurudisha hati hizo za kusafiria kwa mmiliki.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Mahakama inaweza, baada ya kusikiliza pande zote mbili, kukubali au kukataa ombi hilo.

(5) Endapo mtu atashindwa kusalimisha nyaraka zake za kusafiria kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza kukamatwa na kufikishwa Mahakamani na isipokuwa kama Mahakama itaridhika kuwa, hana nyaraka yoyote ya kusafiria, itaamuru kuwa mtu huyo azuiliwe mpaka uchunguzi utakapokamilika wa kosa husika la rushwa au uhujumu uchumi.

(6) Mtu aliyezuiliwa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, ataachiwa ikiwa:

(a) mtu huyo atasalimisha kwa Mamlaka nyaraka zake za kusafiria;

(b) mtu huyo ataithibitishia Mahakama kuwa hana nyaraka yoyote ya kusafiria; au

(c) uchunguzi wa kosa husika la rushwa au uhujumu uchumi umekamilika na Mahakama imeridhika kuwa hakuna mashtaka ya jinai yatakayofunguliwa dhidi yake.

Kumkamata mtu.

**31.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 7 cha Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu au mfanyakazi mwengine yeyote aliyemuidhinisha kwa sababu za msingi, atakuwa na uwezo wa kumkamata mtu yeyote na kupendekeza ashtakiwe kwa kosa chini ya Sheria hii.

Utoaji wa taarifa ambazo zinaweza kuharibu uchunguzi.

**32.-**(1) Mtu, isipokuwa kwa ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu au kwa sababu nyengine ya kisheria, hatatoa maelezo juu ya uchunguzi chini ya Sheria hii ikijumuisha maswali aliyoulizwa wakati wa mahojiano, kitu chochote kilichosalimishwa kwa Mamlaka na utambulisho wa mtu yeyote aliyetajwa wakati wa mahojiano.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Kujifananisha.

**33.** Mtu ambaye sio mfanyakazi wa Mamlaka au mwajiriwa katika taasisi yoyote, na bila ya ruhusa ya Mamlaka au taasisi husika na kwa lengo la kujipatia au kumpatia mtu mwengine manufaa yasiyo halali, akajitambulisha yeye mwenyewe au akafanya kitendo cha kujionesha kwamba yeye ndio au anafanya chini ya uwezo au kazi za mfanyakazi wa Mamlaka au muajiriwa wa taasisi hiyo, ametenda kosa.

Ripoti ya uchunguzi.

**34.**-(1) Mamlaka, baada ya kufanya uchunguzi, itawasilisha ripoti ya matokeo ya uchunguzi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(2) Ripoti ya uchunguzi iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itajumuisha mapendekezo yoyote ya Mamlaka kwamba mtu anaweza kushtakiwa kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi.

Kazi kufanywa kwa nia njema.

**35.**-(1) Mchunguzi au mtu aliyeteuliwa kufanya uchunguzi chini ya masharti ya Sheria hii, atatekeleza kazi na uwezo aliyokasimiwa kwa nia njema na kwa madhumuni ya upatikanaji wa haki.

(2) Endapo kutakuwa na jaribio lolote la ushawishi wa rushwa kwa kutumia nguvu au hadaa kwa Mchunguzi au kwa mtu anayefanya uchunguzi, Mchunguzi au mtu anayefanya uchunguzi huo atatoa taarifa kwa Mkurugenzi Mkuu.

## SEHEMU YA TANO
## MAKOSA YA RUSHWA

Rushwa.

**36.** Mtu ambaye, ikiwa moja kwa moja au vyenginevyo:

(a) anapokea, anaomba au anakubali kupokea au anakubali kuomba faida isiyo halali kwa ajili yake au kwa ajili ya mtu mwengine; au

(b) anatoa, anaahidi au anakubali kutoa au anakubali kuahidi kutoa faida isiyo halali kwa ajili yake au kwa ajili ya mtu mwengine,

ametenda kosa.

Rushwa ya wakala.

**37.**-(1) Kifungu hiki kitatumika kuhusiana na faida ambayo itakuwa kama kishawishi, zawadi au vyenginevyo endapo wakala:

(a) atafanya au ataacha kufanya kitu chochote kinachohusiana na shughuli au kazi za mkuu wa wakala; au

(b) ataonesha au ataacha kuonesha upendeleo au bila ya upendeleo, juu ya kitu chochote ikijumuisha mtu au maombi yanayohusiana na shughuli au kazi za mkuu wa wakala.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, faida iliyopatikana au inayotegemewa ambayo itampelekea wakala kuonesha upendeleo au bila ya upendeleo, itachukuliwa kama kishawishi au zawadi kwa ajili ya kuonesha upendeleo au bila ya upendeleo.

(3) Wakala ambaye:

(a) anapokea, anaomba au anakubali kupokea au anakubali kuomba faida ambayo kifungu hiki kinatumika; au

(b) anatoa, anaahidi au anakubali kutoa au anakubali kuahidi faida ambayo kifungu hiki kinatumika,

ametenda kosa.

Rushwa inayofanywa na Afisa wa umma.

38. Afisa yeyote wa umma ambaye anaomba, anakubali au anapokea faida kutoka kwa mtu mwengine kwa ajili yake binafsi au mtu mwengine kwa lengo la:

(a) kufanya au kuacha kufanya jambo lolote katika kutekeleza kazi au majukumu yake;

(b) kufanya au kuacha kufanya jambo lolote ambalo litawezesha kutekeleza kazi au majukumu yake;

(c) kuharakisha, kuchelewesha, kumuekea vikwazo au kuzuia au kutoharakisha, kutochelewesha, kutozuia utekelezaji wa jambo lolote na afisa mwengine wa umma katika kutekeleza kazi au majukumu yake; au

(d) kumsaidia, kumpendelea, kumzuia au kumchelewesha au kutomsaidia, kutompendelea, kutomzuia au kutomchelewesha mtu mwengine katika miamala ya biashara na taasisi ya umma,

ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini ya mara tatu ya thamani ya faida iliyotolewa au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote viwili.

Rushwa kwa Afisa wa Umma.

**39.** Mtu ambaye atatoa, atakubali kutoa au ataahidi kutoa faida kwa afisa wa umma, kwa ajili ya:

(a) kufanyiwa au kuacha kufanyiwa jambo lolote katika kutekeleza kazi au majukumu yake;

(b) kufanyiwa au kuacha kufanyiwa jambo lolote ambalo litawezesha kutekeleza kazi au majukumu yake;

(c) kuharakishiwa, kucheleweshewa, kumuekea vikwazo au kuzuiliwa au kutoharakishiwa, kutocheleweshewa, kutozuiliwa utekelezaji wa jambo lolote na afisa mwengine wa umma katika kutekeleza kazi au majukumu yake baadae; au

(d) kusaidiwa, kupendelewa, . kuzuiwa au kucheleweshewa au kutosaidiwa, kutopendelewa, kutozuiwa au kutocheleweshewa mtu mwengine katika miamala ya biashara na taasisi za umma.

ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini ya mara tatu ya thamani ya zawadi iliyotolewa au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote viwili.

Kuomba au kupokea faida kinyume na sheria kwa mtu anayefanya au kutekeleza maamuzi ya Mahakama.

**40.**-(1) Afisa yeyote wa Mahakama au mtu mwengine yeyote mwenye ushawishi katika maamuzi ya mahakama ambaye:

(a) anaomba, anapokea au anakubali kupokea faida isiyo halali; au

(b) anaahidi kama sharti la kukamilisha majukumu yake yoyote au kwa ajili ya kuacha kutekeleza jukumu lake la kawaida au kitaalamu,

ili kusababisha matokeo katika maamuzi ambayo yatakuwa yapo kinyume na Sheria, ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "Afisa wa Mahakama" maana yake ni Jaji, Hakimu au muajiriwa mwengine yeyote wa Mahakama au mtu mwengine yeyote mwenye ushawishi katika maamuzi ya Mahakama.

Rushwa katika minada.

**41.** Mtu ambaye, kinyume na sheria:

(a) anaahidi kutoa faida yoyote kwa mtu mwengine yeyote kama kishawishi, zawadi au vyenginevyo kwa ajili ya kumfanya mtu mwengine kuacha au kukusudia kuacha kushiriki katika mnada wowote utakaoendeshwa na au kwa niaba ya taasisi yoyote ya umma; au

(b) anaomba au anapokea faida yoyote kwa mtu mwengine kama kishawishi, zawadi au vyenginevyo kwa ajili ya kumfanya mtu mwengine kuacha au kukusudia kuacha kushiriki katika mnada wowote utakaoendeshwa na au kwa niaba ya taasisi yoyote ya umma,

ametenda kosa.

Ushawishi wa siri katika kutoa ushauri.

**42.**-(1) Mtu ambaye, kinyume na sheria:

(a) anapokea, anaomba au anakubali kupokea au kuomba faida ikiwa mtu huyo anakusudia faida hiyo kuwa ya siri kutoka kwa mtu anayemshauri; au

(b) anatoa, anaahidi kutoa au anakubali kutoa au kuahidi kutoa faida ikiwa mtu huyo anakusudia faida hiyo kuwa ya siri kutoka kwa mtu anayemshauri,

ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kutoa ushauri" inajumuisha kutoa maelezo.

Rushwa kwa ajili ya kutoa msaada kuhusu mkataba.

**43.**-(1) Mtu ambaye, bila ya kuwa na mamlaka ya kisheria au sababu za msingi, anaahidi faida isiyo halali kwa afisa wa umma kama ni kishawishi, zawadi au vyenginevyo kwa lengo la kumfanya afisa huyo wa umma kumpa msaada au kutumia ushawishi katika:

(a) kukuza, kutekeleza au kununua chochote kati ya:

(i) mkataba na taasisi ya umma kwa ajili ya kutekeleza kazi yoyote, kutoa huduma yoyote, kufanya kitu chochote au kusambaza bidhaa ya aina yoyote; au

(ii) mkataba mdogo wa kufanya kazi yoyote, kutoa huduma yoyote, kufanya kitu chochote au kusambaza bidhaa ya aina yoyote iliyotakiwa kufanywa, kutolewa au kusambazwa chini ya mkataba wowote na taasisi ya umma.

(b) malipo ya bei, malipo ya makubaliano au fedha nyengine zilizotolewa au kupatikana vyenginevyo kwa ajili ya mkataba au mkataba mdogo huo,

ametenda kosa.

(2) Afisa wa umma ambaye, bila ya kuwa na mamlaka ya kisheria au sababu za msingi, anaomba au anapokea faida yoyote isiyo halali kama ni kishawishi, zawadi au vyenginevyo kwa kutoa msaada au kutumia ushawishi katika:

(a) kukuza, kutekeleza au kununua; au

(b) malipo ya bei, malipo ya makubaliano, au fedha nyengine zilizotolewa au kupatikana vyenginevyo kwa ajili ya mkataba au mkataba mdogo huo uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki,

ametenda kosa.

Kumdanganya mkuu.

**44**. Wakala ambaye:

(a) anatoa maelezo kwa mkuu wake ambayo anajua kuwa ni ya uongo au yenye kupotosha kwa namna yoyote; au

(b) anatumia au atatoa kwa mkuu wake nyaraka ambazo anajua kuwa zinatoa taarifa za uongo au zinazopotosha na akasababisha hasara kwa mkuu wake,

ametenda kosa.

Mgongano wa maslahi.

**45**.-(1) Endapo wakala:

(a) atakuwa ana maslahi binafsi ya moja kwa moja au vyenginevyo katika maamuzi atakayofanya mkuu wake;

(b) anajua au ana sababu ya kujua kwamba mkuu wake hafahamu kuhusiana na maslahi hayo na wakala akashindwa kuyaeleza maslahi hayo; na

(c) anashiriki katika majadiliano yanayohusiana na uamuzi,

ametenda kosa.

(2) Mkuu anaweza kumuidhinisha wakala wake kupiga kura au kushiriki kupiga kura kwa niaba yake katika kupitisha maamuzi ya taasisi binafsi na kupiga kura au kushiriki kwake kupiga kura haitokuwa kwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Wakala ambaye kwa kujua atajipatia au atazuia manufaa ya moja kwa moja au vyenginevyo yanayohusiana na mikataba, makubaliano au uwekezaji wowote unaotokana au unaohusiana na taasisi kama hali itakavyokuwa, ametenda kosa.

Faida isiyoruhusiwa kwa wadhamini kwa kuteuliwa.

**46.**-(1) Kifungu hiki kitatumika kuhusiana na faida ambayo hupatikana kutokana na kishawishi au zawadi inayohusiana na uteuzi wa mtu kama mdhamini wa mali au kwa kushiriki au kusaidia katika uteuzi huo.

(2) Mtu ambaye:

(a) anapokea, anaomba au anakubali kupokea au kuomba faida kutoka kwa mdhamini wa mali ambayo kifungu hiki kinahusika; au

(b) anatoa, anaahidi kutoa au anakubali kutoa au kuahidi kutoa faida kutoka kwa mdhamini wa mali ambayo kifungu hiki kinahusika,

ametenda kosa.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki hayatotumika katika kitendo chochote kilichofanywa kwa kupata ridhaa ya wanufaika wa mali au kwa mujibu wa amri ya Mahakama.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "mdhamini wa mali" inajumuisha:

(a) mtekelezaji au msimamizi wa mirathi aliyeteuliwa kusimamia mali; au

(b) mtu ambaye, kwa hati ya uwakala, hati ya uteuzi au ajira ana mamlaka ya kusimamia au kutunza mali kwa niaba ya mtu mwengine.

Rushwa ya zabuni.

**47.**-(1) Kifungu hiki kinahusika na faida ambayo ni kishawishi au zawadi kwa:

(a) kuzuia kuwasilisha zabuni, ahadi, ainisho la bei au kuomba zabuni;

(b) kujitoa au kubadilisha zabuni, ahadi, ainisho la bei au kuomba zabuni; au

(c) kuwasilisha zabuni, ahadi, ainisho la bei au kuomba zabuni.

(2) Mtu ambaye:

(a) anapokea, anaomba au anakubali kupokea au kuomba faida ambayo kifungu hiki kinahusika; au

(b) anatoa, anaahidi au anakubali kutoa au kuahidi faida ambayo kifungu hiki kinahusika,

ametenda kosa.

(3) Masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam.11 ya 2016 yatatumika kuhusiana na uchunguzi wa makosa na ufunguaji wa kesi zinazohusiana na makosa ya rushwa katika ununuzi wa vifaa, kazi na utoaji wa huduma za ushauri elekezi katika taasisi za umma.

Matumizi mabaya ya wadhifa.

**48.** Mtu ambaye:

(a) anatumia vibaya nafasi yake katika kutekeleza kazi zake;

(b) anatumia nafasi yake kwa madhumuni ya kupata faida isiyo ya halali kwa ajili yake, kwa mtu mwengine au taasisi; au

(c) anashindwa kutekeleza kazi zake kama anavyotakiwa na sheria,

ametenda kosa.

Uhaulishaji wa mapato ya rushwa.

**49.**-(1) Mtu ambaye:

(a) anabadilisha, anahaulisha au anaondosha mali akijua kuwa mali hiyo inatokana na mapato ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi kwa lengo la kuficha au kubadilisha uhalisia wa mali au kumsaidia mtu yeyote anayejihusisha kufanya makosa hayo kukwepa hatua za kisheria kutokana na vitendo vyake; au

(b) anajipatia, anamiliki au anatumia mali huku akijua kwamba mali hiyo inatokana na mapato ya makosa ya rushwa au uhujumu uchumi,

ametenda kosa.

(2) Endapo Mkurugenzi Mkuu atakuwa na sababu ya kuamini kwamba, mtu yeyote amepokea au amejipatia faida au mali kinyume na sheria, anaweza kutoa taarifa kwa mtu huyo au kwa mtu mwengine yeyote ambaye amepata faida, mali, mapato ya rushwa, thamani ya fedha au sehemu yoyote ya mapato ya rushwa, thamani

ya fedha, faida, mali au fedha inayoaminika kuwa imehaulishwa au kufikishwa na mtu anayetuhumiwa kupokea au kujipatia kinyume na sheria au kimepatikana na wakala wa mtu huyo kwa kumuelekeza asiihaulishe au asiitoe umiliki wa mali au thamani ya fedha hiyo kama ilivyoainishwa katika taarifa.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kutoa taarifa kwa mtu mwengine yeyote ambaye fedha au mali hiyo chini ya kifungu hiki inaweza kupitishwa katika utekelezaji wa sheria.

(4) Taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itaendelea kufanya kazi na kumlazimu mtu ambaye amepewa taarifa kwa kipindi cha miezi sita tokea tarehe ya taarifa hiyo au mwenendo wa kosa lililofunguliwa dhidi ya mtu yeyote chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusiana na faida au mali inayomhusu mtu huyo mpaka shauri hilo litakapoamuliwa.

(5) Mtu ambaye amepewa taarifa na kwenda kinyume na taarifa hiyo chini ya kifungu kidogo cha (2) na (3) vya kifungu hiki, ambaye, atahaulisha, ataondoa mali au thamani ya fedha au asitoe umiliki wa thamani ya fedha au mali iliyoelezwa katika taarifa, ametenda kosa.

(6) Katika uendeshaji wa kosa lolote chini ya kifungu hiki, itakuwa ni utetezi kwa mshtakiwa ikiwa atairidhisha Mahakama kuwa:

(a) kiasi cha fedha au mali nyengine iliyoorodheshwa katika taarifa iliwasilishwa kwa mfanyakazi au kwa mtu mwengine yeyote kama ilivyoelekezwa katika taarifa;

(b) kiasi cha fedha au mali nyengine iliyoainishwa katika taarifa iliyotolewa mahakamani na kuhifadhiwa na Mahakama hiyo; au

(c) taarifa imeondolewa na Mkurugenzi Mkuu kwa taarifa ya maandishi.

Rushwa katika uchaguzi.

**50.**-(1) Mtu ambaye atatoa rushwa kwa mtu mwengine ikiwa moja kwa moja au vyenginevyo kwa lengo la kumshawishi mtu huyo au mtu mwengine yeyote kupiga kura au kuacha kupiga kura, ametenda kosa.

(2) Mpiga kura ambaye atapokea rushwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Rushwa ya Afisa wa kigeni.

**51.**-(1) Mtu ambaye, kwa makusudi, anaahidi au anampa moja kwa moja au vyenginevyo Afisa wa kigeni au Afisa wa jumuiya ya kimataifa faida isiyo ya halali ikiwa kwa ajili yake, kwa mtu mwengine au taasisi kwa madhumuni ya kumfanya Afisa

huyo wa kigeni kutenda au kuacha kutenda jambo wakati wa kutekeleza mahusiano ya kibiashara au kujipatia faida nyengine isiyo halali inayohusiana na shughuli za kiuchumi za kitaifa au kimataifa au muamala wa kibiashara, ametenda kosa.

(2) Afisa wa kigeni au afisa wa jumuiya ya kimataifa ambaye, kwa makusudi, atashawishi au atapokea moja kwa moja au vyenginevyo faida isiyo halali kwa ajili yake au kwa mtu mwengine au taasisi kwa madhumuni ya kumfanya mtu huyo kutenda au kuacha kutenda jambo wakati wa kutekeleza majukumu yake, ametenda kosa.

(3) Afisa wa kigeni au afisa wa jumuiya ya kimataifa ambaye, kwa makusudi na kwa njia ya rushwa atapokea, atashawishi, atatoa, ataahidi au kwa njia ya rushwa atakubali kupokea, kushawishiwa, kutoa au kuahidi faida ikiwa kwa ajili yake au kwa mtu mwengine, ikiwa moja kwa moja au vyenginevyo kwa madhumuni ya kumfanya mtu huyo kutenda au kuacha kutenda jambo wakati wa kutekeleza majukumu yake, ametenda kosa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "afisa wa kigeni" maana yake ni mtu:

(a) anayeshikilia nafasi katika chombo cha kutunga sheria, Ofisi ya Utawala au Mahakama ya nchi ya kigeni ikiwa mtu huyo ameteuliwa au amechaguliwa;

(b) anayefanya kazi za umma za nchi ya kigeni ikijumuisha wakala wa umma au shirika la umma;

(c) aliyeajiriwa na bodi, kamisheni, shirika au chombo chengine au mamlaka ambayo inafanya kazi kwa niaba ya nchi ya kigeni au mfanyakazi wa umma wa kimataifa; au

(d) ambaye ameidhinishwa na jumuiya ya kimataifa kufanya kazi kwa niaba ya jumuiya hiyo.

Kushawishi au kufanya rushwa ya ngono.

**52.**-(1) Mtu ambaye, kwa namna yoyote, atashawishi, atakubali au ataahidi kufanya ngono au atamfanya mtu mwengine akubali au aahidi kufanya ngono kwa ajili ya kupata huduma au kutotoa huduma, ametenda kosa.

(2) Endapo ngono imefanyika kwa ajili ya mnufaika wa ngono hiyo afanye jambo ambalo lipo kinyume na sheria, adhabu yake ni kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba lakini kisichozidi miaka kumi pamoja na faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi na Tano za Kitanzania lakini isiyozidi Milioni Ishirini za Kitanzania.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA YA UHUJUMU UCHUMI

Matumizi mabaya ya mali ya Umma.

**53.**-(1) Mtu aliyepewa dhamana ya kusimamia mali ya umma na akaitumia mali hiyo kwa madhumuni mengine tofauti na yaliyokusudiwa, akaiharibu, akashindwa kuihifadhi au akaitumia kinyume na sheria, ametenda kosa.

(2) Mtu aliyepewa mamlaka ya umma au msimamizi wa utumishi wa umma ambaye atatumia fedha za bajeti ya Serikali au mali nyengine ya umma kwa malengo ambayo hayakukusudiwa bila ya ruhusa ya mamlaka husika, ametenda kosa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "mali ya umma" maana yake ni mali yenye manufaa kwa umma, ikiwa inamilikiwa na:

(a) taasisi;

(b) kampuni;

(c) chama cha ushirika; au

(d) jumuiya zisizo za Serikali zenye kutambulika kisheria.

Matumizi mabaya ya mali na mapato.

**54.**-(1) Mtu ambaye, kwa njia ya udanganyifu au kinyume na sheria:

(a) anajipatia mali, huduma ya umma au faida;

(b) anaweka rehani, anatoza malipo au anaondoa mali yoyote;

(c) anaharibu mali ikijumuisha kusababisha kompyuta au mashine yoyote ya kielektroniki kufanya kazi yoyote moja kwa moja au vyenginevyo ambayo itasababisha hasara au athari katika mapato au huduma yoyote; au

(d) anashindwa kulipa kodi, ada, ushuru au malipo yoyote yanayopaswa kulipwa kwa taasisi ya umma au binafsi au anajipatia msamaha, shufaa, punguzo lolote katika malipo ya kodi, ada, ushuru au malipo,

ametenda kosa.

(2) Afisa au mtu mwengine ambaye anahusika na uendeshaji, uhifadhi, usimamizi, upokeaji au utumiaji wa sehemu yoyote ya mapato au mali, ametenda kosa, ikiwa mtu huyo:

(a) kwa njia ya udanganyifu au kinyume na sheria, atafanya malipo au atafanya malipo ya ziada katika mapato kwa:

(i) bidhaa yenye kiwango kidogo au yenye kasoro;

(ii) bidhaa ambayo haijasambazwa au haijasambazwa kwa ukamilifu; au

(iii) huduma ambayo haikutolewa au haikutolewa ipasavyo.

(b) kwa makusudi, ameshindwa kufuata sheria yoyote, taratibu zinazotumika au miongozo kuhusiana na ununuzi, kupanga, mauzo au utoaji wa mali, kufunga mikataba, usimamizi wa fedha au kujipatia kipato.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "mali" maana yake ni mali yenye kuhamishika au isiyohamishika ikijumuisha fedha za taasisi au zilizo chini ya udhibiti wa taasisi, zinazotokana au kutumiwa na taasisi.

Matumizi mabaya ya mali.

**55.**-(1) Mtu ambaye, kwa njia zisizo halali, anajipatia huduma yoyote ya serikali, faida, mali au mali ya shirika la umma au kampuni binafsi ikiwa ameajiriwa katika taasisi hiyo au vyenginevyo, ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Serikali" inajumuisha Serikali kuu, serikali za mitaa, taasisi ya umma, shirika la umma, mradi au mradi wa shirika lisilo la kiserikali linalofadhiliwa kikamilifu na Serikali au serikali ya kigeni kwa manufaa ya umma.

Kukwepa kodi.

**56.**-(1) Mtu ambaye anakusudia kukwepa kulipa kodi au anasaidia katika kukwepa kodi kwa kutoa au kufanya:

(a) hesabu za uongo;

(b) mabadiliko ya uwongo katika nyaraka yoyote inayohusiana na kodi;

(c) tamko la uwongo au kwa makusudi atapotosha kiwango, ubora, thamani au maelezo yoyote yanayohusiana na bidhaa ambayo inatozwa kodi;

(d) tathmini ya chini ya kodi inayolipwa na afisa anayehusika na tathmini ya kodi; au

(e) kwa njia nyengine yoyote itakayobuniwa kwa madhumuni ya kukwepa kodi,

ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kodi" inajumuisha kodi, ushuru, ada na malipo mengine yoyote yanayotozwa chini ya sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotumika Zanzibar au chini ya kanuni zozote zilizotungwa katika sheria zinazohusika.

Hasara inayotokana na uzembe.

**57.**-(1) Mtu ambaye ameajiriwa au hajaajiriwa katika taasisi ya umma:

(a) anafanya au anaacha kufanya jambo lolote;

(b) anaacha kutekeleza wajibu alionao; au

(c) kwa kushindwa kuchukua tahadhari za msingi au kushindwa kutekeleza majukumu yake katika njia inayofaa, anaisababishia taasisi ya umma kupata hasara ya kifedha au akasababisha uharibifu katika mali yoyote inayomilikiwa na taasisi ya umma au iliyopo katika usimamizi wa taasisi ya umma,

ametenda kosa chini ya kifungu hiki, endapo thamani ya hasara hiyo au uharibifu huo ni zaidi ya Shilingi Milioni Moja za Kitanzania.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi ya umma itahesabika kuwa imepata hasara ya kifedha bila ya kujali kwamba:

(a) imepokea au ina haki ya kupokea malipo yoyote kuhusiana na hasara hiyo chini ya sera yoyote ya bima; au

(b) imelipwa kwa njia yoyote au ina haki ya kulipwa kwa hasara hiyo.

Magendo.

**58.**-(1) Mtu ambaye anasafirisha bidhaa au mali yoyote kwa njia ya magendo kama inavyokatazwa chini ya masharti ya Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Nam. 1 ya 2003 au kanuni zake, ametenda kosa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Nam. 1 ya 2003 au kanuni zake yatatumika kuhusiana na adhabu chini ya Sheria hii.

Kuhodhi.

**59.** Mtu ambaye anahodhi bidhaa yoyote kwa madhumuni ya kuzuia au kudhibiti kusambaza au mzunguko wa bidhaa ili kudhibiti bei ya bidhaa hiyo kwa manufaa yake au ushindani, ametenda kosa.

Kufanya jambo kinyume na ushindani wa soko.

**60.** Mtu ambaye anafanya au anaacha kufanya jambo ambalo ni kinyume na ushindani wa soko kwa lengo la kuzuia ushindani wa soko la bidhaa au huduma, ametenda kosa.

Matumizi mabaya ya taarifa rasmi.

**61.**-(1) Mtu ambaye ameajiriwa katika taasisi yoyote na kwa sababu ya ajira hiyo yupo katika nafasi ya kupata au kujua taarifa sahihi katika zabuni, mauzo, ununuzi, upatikanaji au uondoshaji wa mali yoyote, bidhaa au huduma na akatumia taarifa hizo kwa manufaa yake binafsi au kwa manufaa ya mtu mwengine mwenye maslahi katika zabuni hiyo, mauzo, ununuzi, upatikanaji au uondoshaji wa mali, ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "ajira" inajumuisha ajira ya mkataba na ya kutoa huduma au vyenginevyo, ajira ya muda au ya kudumu au kwa malipo au bila ya malipo ambayo taarifa hizo zimepatikana.

Utakatishaji wa fedha haramu.

**62.**-(1) Mtu ambaye anajihusisha au anafanya jambo linalojumuisha kosa la utakatishaji wa fedha haramu chini ya Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yanayotokana na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009, ametenda kosa.

(2) Bila ya kujali masharti yoyote chini ya Sheria hii, masharti ya Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yanayotokana na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 yatatumika kuhusiana na adhabu chini ya Sheria hii.

Usafirishaji wa dawa za kulevya.

**63.**-(1) Mtu ambaye kwa njia yoyote ambayo ni kinyume na sheria anaingiza, anasafirisha, anatengeneza, anamiliki, ananunua, anauza, anatoa, anasambaza, anahifadhi, anasimamia, anapeleka au anagawa kwa mtu yeyote dawa ya nakotiki au saikotropiki au anaahidi kutoa dawa ya nakotiki au saikotropiki, ametenda kosa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya 2021 na kanuni zake yatatumika kuhusiana na dhamana na adhabu katika kifungu hiki.

Bidhaa, fedha au huduma bandia.

**64.** Mtu ambaye anashiriki moja kwa moja au vyenginevyo katika vitendo vya kughushi bidhaa, fedha au utambulisho wa bidhaa au huduma au anamiliki fedha au bidhaa za kughushi kwa manufaa ya kiuchumi au kibiashara, ametenda kosa.

Biashara ya fedha kinyume na sheria.

**65.**-(1) Mtu ambaye kinyume na sheria anabadilisha au anakusudia kubadilisha bei ya kubadilishia fedha ya kigeni au bila ya halali anabadilisha fedha ya kigeni kwa manufaa yake mwenyewe, mshirika wake au mshirika wa kibiashara ikiwa moja kwa moja au vyenginevyo, ametenda kosa.

(2) Mtu au taasisi itakayofanya biashara yoyote kuhusiana na miamala ya fedha kinyume na sheria, imetenda kosa.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

**Kumzuia Mtumishi.**

**66.** Mtu ambaye:

(a) bila ya sababu za msingi, anamzuia, anamuwekea kikwazo, anamshambulia au anamtishia mtu ambaye anatekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii;

(b) kwa kujua anamdanganya au anampotosha Mkurugenzi Mkuu au mtu anayefanya kazi chini ya Sheria hii;

(c) anaharibu, anabadilisha, anaficha au anaondoa nyaraka, kumbukumbu au ushahidi ambao mtu huyo anaamini au ana sababu za kuamini kwamba unaweza kuwa muhimu kwa uchunguzi au shauri chini ya Sheria hii;

(d) anatoa tuhuma za uongo kwa Mkurugenzi Mkuu au mtu anayefanya kazi chini ya Sheria hii; au

(e) anamtishia Mkurugenzi Mkuu au mtu yeyote anayefanya kazi kwa mujibu wa Sheria hii au Kanuni,

ametenda kosa.

Adhabu ya jumla.

**67.** Mtu ambaye ametiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii na ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyoelezwa kwa kosa hilo:

(a) ikiwa ni kosa la uhujumu uchumi, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Mia Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka ishirini au adhabu zote mbili;

(b) ikiwa ni kosa la rushwa, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na Nne za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka kumi na tano au adhabu zote mbili; au

(c) ikiwa ni kosa jengine, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au

kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba au adhabu zote mbili.

Faini ya ziada ya lazima

**68.**-(1) Mtu atakayepatikana na hatia kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi atalipa faini ya ziada ya lazima ikiwa mtu huyo alipata faida inayoweza kuhesabiwa au mtu yeyote alipata hasara inayoweza kuhesabiwa.

(2) Faini ya ziada ya lazima iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itakuwa:

(a) sawa na mara mbili ya kiasi cha faida au hasara iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki; na

(b) ikiwa ni matendo ambayo yamejumuisha kosa yalisababisha faida na hasara kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, sawa na mara mbili ya jumla ya faida na kiasi cha hasara.

## SEHEMU YA NANE
## FIDIA YA UREJESHAJI WA FAIDA ISIYOFAA

Wajibu wa kulipa fidia.

**69.** Mtu ambaye anafanya jambo lolote ambalo linapelekea kosa la rushwa au uhujumu uchumi atakuwa na wajibu wa kulipa fidia kwa mtu yeyote ambaye atapata hasara kutokana na kiasi ambacho kingefidiwa kwa hasara iliyopatikana.

Wajibu kwa manufaa yasiyofaa.

**70.** Mtu ambaye anapokea faida ambayo itapelekea kuwa ni kosa chini ya kifungu cha 36, 37, 42, 44, 45, 46 au 53 vya Sheria hii atalipa, kwa kiwango cha thamani ya faida kwa watu wafuatao, kama:

(a) upokeaji unapelekea kosa chini ya kifungu cha 37, 44 au 45 vya Sheria hii, kwa mkuu wa wakala;

(b) upokeaji unapelekea kosa chini ya kifungu cha 36 cha Sheria hii, kwa mtu aliyeombwa;

(c) upokeaji unapelekea kosa chini ya kifungu cha 42 cha Sheria hii kwa mtu aliyeshauriwa; au

(d) upokeaji unapelekea kosa chini ya kifungu cha 46 au 53 cha Sheria hii, kwa watu ambao wananufaika na mali hiyo.

Wajibu mbali mbali.

**71.**-(1) Kiwango cha fedha kitakacholipwa kwa taasisi ya umma ambacho mtu aliyefanya kosa chini ya kifungu cha 69 cha Sheria hii, kinaweza kulipwa kwa taasisi ya umma hiyo au kwa Mamlaka kwa niaba yake.

(2) Bila ya kujali masharti yoyote ya Sheria hii, Mamlaka haitazuiliwa kufungua shauri la madai ili kurejesha kiwango cha fedha chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mtu hatostahiki kulipwa kiasi chochote chini ya kifungu cha 69 cha Sheria hii kutokana na matokeo ya rushwa au uhujumu uchumi ikiwa mtu huyo na yeye amefanya kitendo ambacho kinajumuisha rushwa au uhujumu uchumi.

Amri ya fidia baada ya kutiwa hatiani.

**72.**-(1) Mahakama ambayo imemtia hatiani mtu yeyote kwa kosa lolote la rushwa au uhujumu uchumi, wakati wa kumtia hatiani mtu huyo au kwa ombi linalofuata, itamuamuru mtu huyo:

(a) kulipa kiwango chochote cha fedha ambacho mtu huyo anastahiki kulipa chini ya kifungu cha 68 au 69 cha Sheria hii; au

(b) kumpa mmiliki halali:

(i) mali yoyote iliyopatikana katika mwenendo au iliyotokana na kitendo ambacho kinajumuisha kosa la rushwa au uhujumu uchumi; au

(ii) kiwango cha fedha kinacholingana na thamani ya mali hiyo.

(2) Endapo kutakuwa hakuna mmiliki halali chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) cha kifungu hiki, Mahakama itaamuru kwamba mali au kitu chenye thamani ya mali hiyo kitaifishwe kwa Serikali.

(3) Katika kutoa amri chini ya kifungu hiki, Mahakama inaweza kuweka kiwango cha fedha au kuamua kiwango chochote cha fedha kinachostahiki kuwekwa.

(4) Amri chini ya kifungu hiki inaweza kutekelezwa na mtu ambaye amefaidika na amri hiyo, kama ambavyo amri hiyo imetolewa chini ya shauri la madai.

Kutaifisha mali ambayo haina maelezo.

**73.**-(1) Mamlaka inaweza, kwa kuzingatia masharti ya sheria inayohusika, kufungua shauri chini ya kifungu hiki dhidi ya mtu ikiwa:

(a) Mamlaka imeridhika kwamba, mtu huyo anayo mali ambayo ameshidwa kuitolea maelezo; au

(b) mtu huyo amepewa muda wa kutosha ili kueleza uwiano baina ya mali husika na mapato yake na Mamlaka haikuridhika.

(2) Mashauri chini ya kifungu hiki yatafunguliwa Mahakama Kuu kwa njia ya maombi maalum.

(3) Endapo Mamlaka itatoa ushahidi kwamba mtu anayo mali isiyokuwa na maelezo, Mahakama itamtaka mtu huyo kutoa ushahidi utakaoiridhisha Mahakama kwamba mali alizonazo hakuzipata kwa njia ya rushwa au uhujumu uchumi.

(4) Endapo Mahakama haikuridhika na ushahidi uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, inaweza kuamuru mtu huyo kulipa Serikalini kiwango cha fedha kilicho sawa na thamani ya mali isiyokuwa na maelezo.

(5) Kwa madhumuni ya mwenendo wa mashauri chini ya kifungu hiki, mali za mtu ambaye mali zake zinatuhumiwa zitajumuisha mali zozote za mtu mwengine yeyote ambaye Mahakama itaona kwamba:

(a) zipo kama dhamana kwa mtu ambaye mali zake zinatuhumiwa au vyenginevyo kwa niaba yake; au

(b) zimepatikana kutoka kwa mtu ambaye mali zake zinatuhumiwa bila ya kutegemea kitu.

(6) Taratibu za kutoa ushahidi, kuhoji shahidi na mambo mengine ya mwenendo wa mashauri chini ya kifungu hiki yatafanywa kwa mujibu wa sheria zinazohusika.

Utaifishaji wa mali.

**74.**-(1) Endapo mtuhumiwa ametiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii, Mahakama inaweza kutoa amri ya kutaifisha kwa kitu au mali yoyote iliyotumika kwa madhumuni ya kutenda kosa au kuwezesha kutendeka kwa kosa au imehusika vyenginevyo katika kutendeka kwa kosa.

(2) Endapo mtu aliyetiwa hatiani siyo mmiliki wa kitu au mali hiyo inayotakiwa kutaifishwa na mmiliki hajulikani alipo au hawezi kupatikana amri ya utaifishaji haitofanyika mpaka masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki yametimizwa.

(3) Amri ya kutaifisha kitu au mali haitotekelezwa mpaka:

(a) kwa taarifa ya siku thelathini ya dhamira ya kutaifisha kitu au mali imetolewa; na

(b) taarifa iliyotolewa katika aya (a) ya kifungu hiki imemaliza muda bila ya zuio lolote lililotolewa au zuio lililowekwa limeondoshwa na Mahakama yenye uwezo.

(4) Endapo kitu au mali itakuwa ni yenye kuharibika mapema na kuuzwa kwa kitu au mali hiyo ni muhimu kwa usimamizi mzuri wa kitu au mali hiyo, Mahakama inaweza kutoa amri ya uuzaji wa kitu au mali hiyo.

(5) Mtu ambaye anadai haki katika kitu au mali iliyotaifishwa chini ya Sheria hii, anaweza kupeleka ombi Mahakamani la kupinga amri ya utaifishaji huo.

Amri ya kuzuia mali inayotuhumiwa.

**75.**-(1) Kwa ombi la upande mmoja la Mkurugenzi Mkuu, Mahakama inaweza kutoa amri ya kukataza uhaulishaji, uondoshaji au ushughulikiaji mwengine wa mali ambayo kuna ushahidi kwamba ilipatikana kwa kitendo cha rushwa.

(2) Endapo mtuhumiwa atakuwa chini ya uchunguzi kutokana na kosa la rushwa au uhujumu uchumi, kwa ombi la Mkurugenzi Mkuu, Mahakama kwa kuzingatia masharti na muda ulioombwa au vyenginevyo kama itakavyoona inafaa, inaweza kutoa amri ya:

(a) uzuiaji wa fedha zote zinazomilikiwa na mtu aliyetajwa katika amri hiyo na mali nyengine zinazodaiwa au zinazomilikiwa na au kwa niaba ya mtuhumiwa; na

(b) kumkataza mtuhumiwa au mtu mwengine yeyote anayefanya kazi kwa niaba yake au mtu mwengine yeyote aliyetajwa katika amri, kuhaulisha, kuweka rehani au kuuza katika njia yoyote pesa au mali iliyozuiliwa.

(3) Mahakama inaweza, kwa kuzingatia amri yoyote iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuainisha fedha, mishahara, ujira, pencheni au mafao mengine anayoyapata mtuhumiwa yanayoonesha chanzo, namna na mazingira ya ulipaji au upokeaji.

(4) Amri chini ya kifungu hiki inaweza kutolewa dhidi ya mtu ambaye amehusishwa na kitendo cha rushwa au dhidi ya mtu aliyejipatia mali ya rushwa.

(5) Katika kutoa amri chini ya kifungu hiki, Mahakama inaweza kuidhinisha:

(a) ulipaji wa madeni yaliyopatikanwa kwa nia njema na kutokana na wadai wa mtuhumiwa, kabla ya maombi ya amri hayajafanywa na Mkurugenzi Mkuu; au

(b) uuzaji, uhaulishaji au uondoaji wa mali yoyote ya mtuhumiwa endapo Mahakama imejiridhisha kwamba, uuzaji, uhaulishaji ni muhimu ili kulinda haki za wengine ambao wanadai kuwa wanamaslahi na mali hiyo.

(6) Amri chini ya kifungu hiki itadumu kwa kipindi cha miezi sita na inaweza kuongezwa muda na Mahakama kwa maombi ya Mamlaka.

(7) Mtu aliyepewa amri chini ya kifungu hiki anaweza kuiomba Mahakama ndani ya siku kumi na tano baada ya kupewa amri hiyo, kukubaliana au kutofautiana na amri hiyo na Mahakama inaweza baada ya kusikiliza pande zote, kukubaliana au kutofautiana na amri au kuliondoa ombi hilo.

(8) Mahakama inaweza kukubali au kutofautiana na amri chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki ikiwa Mahakama itaridhika kwamba, mali inayohusika haikupatikana kutokana na kitendo cha rushwa.

(9) Amri chini ya kifungu hiki, kwa kuzingatia masharti yoyote kinyume na yaliyowekwa chini ya kifungu hiki, itaendelea kutumika:

(a) mpaka Mkurugenzi Mkuu atakapoamua kutoendelea na shauri liliyopo au linalotarajiwa kuwepo chini ya kifungu hiki;

(b) mpaka maamuzi ya mwisho ya shauri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki; au

(c) katika hali ya kutiwa hatiani, mpaka amri ya kutaifisha itakapotolewa na Mahakama chini ya vifungu vya 72 na 73 vya Sheria hii au shauri lolote linalohusiana na hilo kukamilika.

(10) Mtu ambaye amepewa amri chini ya kifungu hiki na kwenda kinyume na amri hiyo, ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili.

Maombi amri ya uzuiaji.

**76.**-(1) Endapo Mahakama itaridhika, kwa maombi yaliyofanywa na Mamlaka, kwamba Mamlaka ina sababu za msingi za kumtuhumu mtu kufanya kosa chini ya Sheria hii na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yanayotokana na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 inaweza ikatoa amri ya kuzuia.

(2) Amri ya kuzuia itakayotolewa chini ya kifungu hiki:

(a) itakabidhiwa mikononi kwa mtu yeyote aliyetajwa katika amri hiyo, ikiwa mtu huyo ndiye mtuhumiwa husika au siyo mtuhumiwa;

(b) itamtaka mtu aliyetajwa katika amri kutangaza kwa maandishi kwa Mamlaka ndani ya saa arubaini na nane ya kutolewa kwa amri hiyo, asili na chanzo cha fedha na mali nyengine zilizozuiliwa; na

(c) itamzuia mtu huyo kuhaulisha, kuweka rehani au kuondosha kwa njia yoyote fedha au mali nyengine zilizotajwa kwa njia yoyote isipokua iwe kwa namna inayoweza kuelezwa katika amri.

Amri ya zuio.

**77.**-(1) Amri ya zuio itatolewa kwa kila mtu aliyetajwa katika amri hiyo.

(2) Endapo Mahakama itaridhika kwamba, Mamlaka imepata au inategemea kupata taarifa mpya muhimu kuhusiana na kosa chini ya Sheria hii, Mahakama inaweza kuihuisha amri ya uzuiaji kwa kipindi cha miezi sita kufuatia ombi la Mamlaka.

(3) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, amri ya uzuiaji itabaki kuwa halali kwa siku sitini kuanzia tarehe iliyotolewa, isipokuwa iwe imefutwa na Mahakama.

(4) Endapo Mamlaka itairidhisha Mahakama kwamba mtuhumiwa yupo nje ya Zanzibar kwa muda wowote, muda ambao mtuhumiwa yupo nje ya Zanzibar hautohesabiwa kama ni sehemu ya muda halali wa amri ya zuio.

Ukamataji wa mali inayohamishika.

**78.**-(1) Endapo wakati wa uchunguzi chini ya Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu atajiridhisha kwamba mali inayohamishika inahusika au inahusishwa na kosa chini ya Sheria hii, anaweza kukamata mali hiyo.

(2) Mkurugenzi Mkuu ataweka kumbukumbu za mali alizozikamata chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na atampatia nakala za kumbukumbu hizo mtu ambaye mali yake imekamatwa.

(3) Ukamataji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatekelezwa kwa kuihifadhi mali iliyokamatwa chini ya usimamizi wowote kama Mkurugenzi Mkuu atakavyoamua.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, endapo Mkurugenzi Mkuu ataona haitowezekana kuiondoa mali aliyoizuia kutoka katika eneo iliyopo, anaweza kuiacha mali hiyo chini ya usimamizi wa mtu aliyekutwa nayo kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu atakavyoelekeza.

(5) Endapo mali inayohamishika imekamatwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ipo chini ya usimamizi wa mtu wa tatu, Mkurugenzi Mkuu anaweza kumpa maelekezo mtu huyo wa tatu asiiondoe mali hiyo bila ya ruhusa yake ya maandishi..

Urejeshaji wa fedha na mali nyenginezo.

**79.**-(1) Fedha zozote zitakazopatikana na Mamlaka zitalipwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali.

(2) Mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika iliyopatikana wakati wa uchunguzi au baada ya uchunguzi kukamilika, baada ya kuanza kwa shauri Mahakamani ikiwa la madai au jinai au baada ya kumalizika kwa mashauri hayo, itakabidhiwa kwa Msajili wa Hazina.

Mashauri yanayotokana na utaifishaji.

**80.**-(1) Endapo amri ya kutaifisha mali imetolewa kulingana na kifungu cha 73 cha Sheria hii, mtu aliyehukumiwa au mtu mwengine yeyote ambaye anadai maslahi katika mali hiyo anaweza, yeye mwenyewe, kufungua shauri Mahakamani kwa kueleza kwamba mali hiyo haitokani na makosa ya rushwa au uhujumu uchumi.

(2) Ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litawasilishwa katika masjala ya Mahakama si zaidi ya miezi mitatu tokea tarehe iliyotangazwa utaifishaji, vyenginevyo amri ya kutaifisha itakuwa ndio ya mwisho.

(3) Mahakama, baada ya kusikiliza ombi, inaweza:

(a) kutoa ombi na kuifuta amri ya utaifishaji au sehemu yoyote ya amri hiyo; au

(b) kuondoa ombi na kuthibitisha amri ya utaifishaji ambayo itakuwa ndio maamuzi ya mwisho.

(4) Endapo Mahakama itakubali ombi chini ya kifungu kidogo cha (3)(a) cha kifungu hiki kuhusiana na mali yoyote iliyotaifishwa, utaifishaji huo utasita na mali hiyo itarudi kwa aliyeshinda shauri kufuatia maamuzi ya Mahakama na muombaji atakuwa na haki ya kurejeshewa mali yake kwa mujibu wa maamuzi ya mahakama.

Malipo mbadala wa kufilisi.

**81.** Endapo Mahakama itajiridhisha kwamba, amri ya utaifishaji mali iliyotolewa chini ya kifungu cha 73 na 74 cha Sheria hii haiwezi kutekelezeka na kwamba mali hiyo:

(a) kwa bidii, haiwezi kujulikanwa ilipo;

(b) imehaulishwa kwa mtu wa tatu katika mazingira ambayo yanaonesha kwamba kuhaulishwa huko kulikua ni kwa madhumuni ya kuepusha kutaifishwa kwa mali hiyo;

(c) ipo nje ya Zanzibar;

(d) imepungua thamani kwa kiasi kikubwa na kuipelekea kuwa haina thamani; au

(e) imechanganywa na mali nyengine ambayo haiwezi kugawanywa kwa urahisi,

inaweza, kumuagiza mtu kulipa kiwango cha thamani sawa na mali, sehemu ya mali au maslahi yake.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI KUHUSU USHAHIDI

Mali isiyo na maelezo kuwa ushahidi wa nyongeza.

**82.**-(1) Mali isiyokuwa na maelezo inaweza kuchukuliwa na Mahakama kuwa ni ushahidi wa nyongeza kwamba mtuhumiwa wa kosa la rushwa au uhujumu uchumi amepokea faida.

(2) Kwa madhumuni ya Sheria hii, "mali isiyokuwa na maelezo" itachukuliwa kuwa ni mali yoyote ya mtuhumiwa na itajumuisha mali yoyote ya mtu mwengine ikiwa Mahakama itabaini kwamba:

(a) inashikiliwa kwa dhamana au vyenginevyo kwa niaba ya mtuhumiwa; au

(b) imepatikana kutoka kwa mtuhumiwa bila ya kuwa na mategemeo yoyote.

Hati ya kuonyesha thamani ya mali.

**83.**-(1) Katika mashtaka ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi au mashauri mengine chini ya Sheria hii, hati ya Afisa Tathmini ambayo inaonesha thamani au faida ya mali itakubalika kama ushahidi na itakuwa ni uthibitisho wa thamani isipokuwa kama itathibitika vyenginevyo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "Afisa Tathmini" maana yake ni mtu aliyeteuliwa, aliyeajiriwa au aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu au Serikali kutia thamani mali na ambaye uteuzi, ajira au uidhinishwaji wake umetangazwa katika Gazeti Rasmi.

Kanuni na taratibu kuhusiana na mshirika wa kosa.

**84.** Kwa madhumuni ya kanuni au utaratibu wowote unaohitaji ushahidi wa nyongeza kwa mshirika; mtu atachukuliwa kama mshirika wa kosa chini ya Sheria hii ikiwa mtu huyo:

(a) anapokea, anashajihisha au anakubali kupokea au anashajihisha kupokea faida kutoka kwa mshtakiwa; au

(b) anaahidi au anakubali kutoa au kuahidi faida kwa mshtakiwa.

Hati inayoonesha ofisi.

**85.** Katika mashtaka ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi au shauri chini ya Sheria hii, hati inayoonesha nafasi ya Afisa au manufaa yake katika taasisi itakubalika Mahakamani kama ushahidi na utakua uthibitisho wa nafasi au manufaa ikiwa utakosekana ushahidi unaothibitisha vyenginevyo.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Mamlaka.

**86.**-(1) Fedha na rasilimali za Mamlaka zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi; na

(b) misaada, michango na fedha nyengine itakayopokea Mamlaka kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika.

(2) Miamala yote ya fedha ya Mamlaka itafanywa na itaongozwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, kanuni zake na sheria nyengine yoyote ya fedha inayohusika.

Ripoti

**87.**-(1) Mamlaka itakuwa na fungu lake la bajeti ambalo litatumika kupitishia na kufanya matumizi ya fedha za Mamlaka.

(2) Naibu Mkurugenzi Mkuu, kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa na atawasilisha kwa Waziri bajeti ya mapato na matumizi ya Mamlaka ya mwaka ujao wa fedha.

(3) Bajeti itaandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, kanuni zake na miongozo itakayotolewa na Serikali kila baada ya muda.

Hesabu na ukaguzi.

**88.**-(1) Mamlaka itaweka au itawezesha kuwekwa vitabu na kumbukumbu sahihi za hesabu za mapato, matumizi, mali na madeni yake.

(2) Hesabu za mwaka za Mamlaka zitatayarishwa na kukaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, kanuni zake na sheria nyengine yoyote ya fedha inayohusika.

Kufungua akaunti ya benki.

**89.** Mamlaka, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, itafungua akaunti ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MASHARTI MENGINEYO

Ripoti ya mwaka.

**90.**-(1) Mamlaka itaandaa ripoti ya kila mwaka na itaiwasilisha kwa Rais ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka husika.

(2) Ripoti ya mwaka itajumuisha maelezo kuhusu kazi zilizofanywa na Mamlaka.

(3) Rais, baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atamuidhinisha Waziri kuiwasilisha ripoti hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Ushughulikiaji wa tuhuma dhidi ya mfanyakazi.

**91**. Endapo kuna tuhuma ya utendaji wa kosa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote kwa mfanyakazi, tuhuma hizo zitashughulikiwa kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa chini ya Sheria hii.

Kumsaidia mtu kutenda kosa.

**92**. Mtu ambaye kwa makusudi atashiriki katika kutoa ushauri, kuficha au kusaidia katika kufanyika kwa kosa chini ya Sheria hii, ametenda kosa.

Ushughu-likiaji wa mali iliyote-lekezwa.

**93.**-(1) Mkurugenzi Mkuu au mfanyakazi mwengine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na Mkurugenzi Mkuu atasimamia na kutoa hesabu au maelezo yake kwa Mahakama kuhusiana na mali zote zilizotelekezwa na ambazo zimechukuliwa na Mamlaka kutokana na makosa ya rushwa na uhujumu uchumi chini ya Sheria hii.

(2) Endapo mali ambayo imetelekezwa si fedha, mali inayohitaji kuuzwa kwa kuhofia kuharibika, na wala si mali inayohitaji kuuzwa kwa haraka kwa manufaa ya mmiliki, Mahakama itaizuia au kutoa amri ya kuzuiliwa kwa mali hiyo na itatoa taarifa na kuagiza kubandikwa katika sehemu ya wazi mahakamani na katika Mamlaka na kumtaka mtu yeyote ambaye anaweza kuwa na madai hayo kufika na kuthibitisha madai yake ndani ya miezi sita kutoka tarehe ya taarifa hiyo.

(3) Endapo thamani ya mali iliyotelekezwa inazidi Shilingi Milioni Moja za Kitanzania, Mahakama pia itatayarisha taarifa kama hiyo ambayo itachapishwa katika gazeti ambalo lina mzunguko mkubwa ndani ya Zanzibar na taarifa hiyo itakuwa na tarehe sawa kama taarifa iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(4) Endapo hakuna mtu aliyeanzisha madai yoyote ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya taarifa, mali ambayo imetelekezwa inaweza kutolewa kwa amri ya Mahakama kama itakavyoona inafaa.

(5) Endapo Mahakama inaona kwamba mali iliotelekezwa inaweza kuoza kwa haraka au inahitaji kuuzwa kwa manufaa ya mmiliki, itaizuia au kutoa amri ya kuzuia na inaweza wakati wowote kuelekeza kwamba iuzwe au iharibiwe bila ya kutoa notisi na baada ya mauzo au uharibifu huo, Mahakama itatoa amri ya notisi ya mauzo au uharibifu huo itolewe kwa utaratibu ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hiki.

(6) Baada ya kukamilika kwa uuzaji au uharibifu uliotajwa chini ya vifungu vidogo vya (4) na (5) vya kifungu hiki, haki ya kuchukua hatua za kisheria kwa ajili ya kurejesha mali ambayo imetelekezwa au mapato ya mauzo hayo itasita.

(7) Mapato ya mauzo ya mali iliyotelekezwa ama yatalipwa kwa mtu ambaye amethibitisha madai yake au kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali.

(8) Endapo mali kama iliyotelekezwa itajumuisha fedha, itashughulikiwa kwa taratibu zote kama ni mapato ya mauzo yaliyoagizwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vidogo vya (2) na (5) vya kifungu hiki.

Kusimamishwa kazi kwa kushtakiwa kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi.

94. Masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 yatatumika kwa Afisa wa Umma ambaye ameshtakiwa au kutiwa hatiani kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi chini ya Sheria hii.

Mfanyakazi kuchukuliwa kama Afisa wa Chuo cha Mafunzo.

95. Endapo mfanyakazi anatekeleza majukumu ya Afisa wa Chuo cha Mafunzo, mfanyakazi huyo, akiwa katika kazi yoyote kama hiyo, atachukuliwa kuwa Afisa wa Chuo cha Mafunzo na atakuwa na uwezo, ulinzi na stahiki zinazohusiana na Afisa huyo.

Kutokuwa na sifa kwa mtu aliyetiwa hatiani.

96. Mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa la rushwa au uhujumu uchumi chini ya Sheria hii hatokuwa na sifa za kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nyadhifa yoyote kwa kipindi cha miaka mitano tokea tarehe aliyotiwa hatiani.

Kutangazwa kwa mtu aliyepatikana na hatia ya rushwa au uhujumu uchumi.

97. Mamlaka, angalau mara moja kwa kila mwaka, itatangaza au itasababisha kutangazwa katika Gazeti Rasmi majina ya watu wote waliopatikana na hatia kwa makosa ya rushwa au uhujumu uchumi chini ya Sheria hii.

Kulindwa kwa mtoa taarifa.

**98.**-(1) Hatua au shauri ikijumuisha hatua ya kinidhamu halitafunguliwa dhidi ya mtu kuhusiana na:

(a) msaada uliotolewa na mtu huyo kwa Mamlaka au Mchunguzi; au

(b) kufichua taarifa dhidi ya mtu yeyote kwa Mamlaka au Mchunguzi.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatatumika kuhusiana na taarifa iliyotolewa na mtu ambaye hana sababu za kuamini kuwa taarifa hiyo ni ya kweli.

(3) Katika mashtaka ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi au mashauri mengine chini ya Sheria hii, shahidi hatatakiwa kubainisha au kutoa taarifa inayoweza kupelekea kutambuliwa kwa mtu aliyesaidia au aliyetoa taarifa kwa Mamlaka au Mchunguzi.

(4) Katika mashtaka ya kosa la rushwa au uhujumu uchumi au mashauri mengine chini ya Sheria hii, Mahakama itahakikisha kwamba taarifa zinazotambulisha au zinazoweza kupelekea kutambuliwa kwa mtu aliyesaidia au aliyetoa taarifa kwa Mamlaka au Mchunguzi zinaondolewa au kufichwa kutoka katika nyaraka zozote ambazo zitatolewa au kukaguliwa kuhusiana na shauri hilo.

(5) Taarifa inayohusiana na kutendeka kwa kosa chini ya Sheria hii haitakubaliwa kuwa ushahidi katika shauri lolote la madai au jinai na hakuna shahidi katika shauri lolote la madai au jinai atakayelazimika:

(a) kutaja jina au anuani ya mtoa taarifa ambaye ametoa taarifa kwa Mamlaka kuhusiana na kosa chini ya Sheria hii au jina au anuani ya mtu yeyote ambaye ameisaidia Mamlaka kwa namna yoyote kuhusiana na kosa hilo; au

(b) kujibu swali lolote, ikiwa jibu la swali hilo litapelekea au litaelekea kugunduliwa kwa jina au anuani ya mtoa taarifa huyo.

(6) Mahakama, endapo jina, anuani au maelezo ya mtoa taarifa au mtu aliyetajwa katika kitabu au waraka ambao unahusika na ushahidi au unahitajika kwa ajili ya uchunguzi katika shauri lolote la jinai au madai ambayo itapelekea kugundulika kwa mtoa taarifa au mtu mwengine kwa jamii, itatoa amri ya kufichwa au kufutwa kwa taarifa hizo ili zisijulikane kwa umma kwa ajili ya kumlinda mtoa taarifa au mtu huyo asitambulike katika jamii.

(7) Mtoa taarifa yeyote ambaye ataekewa kisasi, atadhalilishwa, ataumizwa au atadhuriwa na mtu yeyote anayetuhumiwa kwa kosa la rushwa au wahusika wa makosa ya rushwa, atapewa ulinzi, fidia na msaada unaostahili na Serikali baada ya Mamlaka kuthibitisha ukubwa wa kudhalilishwa, majeraha au madhara aliyoyapata.

Kulindwa kwa shahidi.

**99.**-(1) Shahidi katika shauri lolote kwa kosa chini ya Sheria hii, hatochukuliwa kuwa ni mshiriki wa kosa kwa sababu tu ya kupokea, kutoa, kufanya malipo au kulipwa faida yoyote yeye mwenyewe au kwa niaba yake au kutoka kwa mtuhumiwa.

(2) Endapo mtu:

(a) anafichua kwa Mamlaka kwamba, mtu, afisa wa umma, shirika au taasisi ya umma inahusika au imehusika katika kitendo cha rushwa; na

(b) anaamini kwa sababu za msingi kwamba, taarifa anazotoa zinaweza kuwa za kweli na ni za namna inayopelekea uchunguzi ufanyike chini ya Sheria hii,

hatawajibika kwa madai au jinai kutokana na kufichua taarifa hiyo.

(3) Mtu ambaye atamdhalilisha mtu ambaye ametoa taarifa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno "kudhalilisha" maana yake ni kitendo:

(a) ambacho kinasababisha majeraha, uharibifu au hasara;

(b) cha vitisho au unyanyasaji;

(c) cha ubaguzi, hasara au dharau kuhusiana na ajira ya mtu; au

(d) cha vitisho vya kulipiza kisasi.

Wajibu wa kuripoti faida.

**100.**-(1) Mkuu wa taasisi ambaye ametolewa taarifa na afisa wake kwamba amepokea au ameahidiwa kupewa faida kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii, atatoa taarifa ya faida pamoja na jina ikiwa linajulikana la mtu aliyetoa faida hiyo kwa Mamlaka.

(2) Mtu ambaye atashawishiwa au kuombwa kutoa, atapewa au ataahidiwa kupewa faida au atajaribiwa kushawishiwa au kuombwa, kupewa au kuahidiwa faida

hiyo kinyume na masharti ya Sheria hii, haraka iwezekanavyo, atatoa taarifa kwa Mamlaka kuhusiana na ombi la kutoa, kupata au kukusudia kupata faida pamoja na jina kama linajulikana la mtu aliyemuomba, aliyepata au aliyekusudia kupata faida hiyo kwake.

(3) Mtu ambaye atashindwa, bila ya sababu za msingi kufuata masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Saba za Kitanzania au kifungo cha miaka mitano au adhabu zote mbili.

Kinga kwa mfanyakazi.

**101.** Mfanyakazi hatashtakiwa binafsi kwa kitendo au jambo alilofanya au kuacha kufanya, iwapo alifanya au aliacha kufanya kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Mila sio utetezi.

**102.** Kwa madhumuni ya mashtaka chini ya Sheria hii, kupokea, kuomba au kushawishi kutoa au kuahidi faida yoyote kwamba ni mila inayotumika katika eneo, biashara, ofisi au taaluma haitatumika kama ni utetezi.

Kutowezekana au kutokuwa na nia sio utetezi.

**103.** Katika uendeshaji wa mashtaka kwa makosa chini ya Sheria hii ambayo yanajumuisha faida ambayo ni kishawishi au zawadi kwa kufanya au kuacha kufanya jambo, haitokuwa utetezi kwamba kufanya au kuacha kufanya jambo:

(a) hakukuwa ndani ya uwezo wa mtu au kwamba mtu huyo hakukusudia kufanya au kuacha kufanya; au

(b) hakukutokea.

Mashirikiano na mamlaka nyengine.

**104.**-(1) Mamlaka itaanzisha na kuendeleza mfumo wa mashirikiano na mashauriano na vyombo vya kutekeleza sheria na mamlaka nyengine ndani ya Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, za kikanda na kimataifa zinazohusika na upelelezi na mashtaka, na inaweza kwa dhumuni hilo:

(a) kutoa kinga ya kutoshitakiwa kwa mtu ambaye anatoa ushirikiano katika upelelezi au mashtaka ya kosa chini ya Sheria hii;

(b) kuijulisha mamlaka, kwa juhudi zao wenyewe, endapo kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kosa lolote chini ya Sheria hii limetendeka; na

(c) kwa ombi, kutoa kwa mamlaka taarifa zote muhimu.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, mtu atatoa ushirikiano ikiwa mtu huyo:

(a) ametoa taarifa za ukweli zinazomuhusu au za mtu mwengine juu ya mambo yote muhimu yanayohusiana na matendo yaliyopita ya rushwa na uhujumu uchumi;

(b) amelipa, ameweka au amerejesha kwa hiari mali yote aliyopata kupitia rushwa au uhujumu uchumi; na

(c) amelipia hasara zote zilizotokana na mwenendo wake wa rushwa kwa mali ya umma.

Mashirikiano na sekta binafsi.

**105**. Mamlaka itaanzisha na kudumisha mfumo wa mashirikiano na sekta binafsi na zaidi taasisi za fedha, wakandarasi, washauri elekezi na wasambazaji wa bidhaa au huduma kuhusu masuala yanayohusu kutendeka kwa makosa chini ya Sheria hii na kuhimiza sekta binafsi kutoa taarifa kwa Mamlaka juu ya kutendeka kwa kosa lolote chini ya Sheria hii.

Msaada wa nje.

**106**.-(1) Msaada wa kisheria kuhusiana na kosa la rushwa, uhujumu uchumi na makosa mengine yanayohusiana na hayo, utafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Kusaidiana katika Makosa ya Jinai [Sura 254].

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Sehemu hii, nchi ya kigeni au Serikali inaweza kutoa taarifa ambazo zinaweza kusaidia Mamlaka katika kuanzisha au kufanya uchunguzi, mashtaka, mwenendo wa kimahakama na taarifa kuhusu mali iliyotokana na kosa.

Kubadilishana wahalifu.

**107**. Masuala ya kubadilishana wahalifu kuhusiana na makosa ya rushwa, uhujumu uchumi na makosa mengine yanayohusiana na hayo yatashughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Kubadilishana Wahalifu [Sura 368].

Kitendo kilichofanywa nje ya Zanzibar.

**108**. Kitendo kilichofanywa na mtu nje ya Zanzibar, kitakuwa ni kosa chini ya Sheria hii, ikiwa kitendo hicho kingekuwa ni kosa sawa na kwamba kitendo hicho kimefanyika Zanzibar.

Ufunguaji wa mashtaka.

**109**.-(1) Mkurugenzi Mkuu au mtu **yeyote** atakayeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu na kwa ruhusa ya Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kuendesha mashtaka ya makosa chini ya Sheria hii.

(2) Shtaka kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, halitoanzishwa na Mamlaka isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mahakama za usikilizaji wa mashauri.

**110**. Makosa yaliyotajwa chini ya Sheria hii yatagawanywa kama kosa la uhujumu uchumi, kosa la rushwa na makosa mengine na yatasikilizwa katika Mahakama kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Sheria hii.

Kanuni.

**111**. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Miongozo.

**112**. Mkurugenzi Mkuu anaweza kuandaa kanuni za maadili na miongozo ya Mamlaka kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Mamlaka.

Kufuta na kubakiza.

**113**.-(1) Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Nam.1 ya mwaka 2012 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii litaendelea na kuchukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, suala lolote liliyopo Mahakamani kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litashughulikiwa na kutatuliwa chini ya Sheria iliyofutwa.

JADWELI

MAKOSA NA MAHAKAMA ZITAKAZOSIKILIZA

[Chini ya kifungu cha 110]

A. MAKOSA YA UHUJUMU UCHUMI

| KIFUNGU | KOSA | MAHAKAMA |
|---|---|---|
| 53 | Matumizi mabaya ya mali ya umma. | Mahakama Kuu |
| 54 | Matumizi mabaya ya mali na mapato. | Mahakama Kuu |
| 55 | Matumizi mabaya ya mali. | Mahakama Kuu |
| 56 | Kukwepa kodi. | Mahakama Kuu |
| 57 | Hasara inayotokana na uzembe. | Mahakama Kuu |
| 58 | Magendo. | Mahakama Kuu |
| 59 | Kuhodhi. | Mahakama Kuu |
| 60 | Kufanya jambo kinyume na ushindani wa soko. | Mahakama Kuu |
| 61 | Matumizi mabaya ya taarifa rasmi. | Mahakama Kuu |
| 62 | Utakatishaji wa fedha haramu. | Mahakama Kuu |
| 63 | Usafirishaji wa dawa za kulevya. | Mahakama Kuu |
| 64 | Bidhaa, fedha au huduma bandia. | Mahakama Kuu |
| 65 | Biashara ya fedha kinyume na sheria. | Mahakama Kuu |

## B. MAKOSA YA RUSHWA

| KIFUNGU | KOSA | MAHAKAMA |
|---|---|---|
| 36 | Rushwa. | Mahakama ya Mkoa |
| 37 | Rushwa ya wakala. | Mahakama ya Mkoa |
| 38 | Rushwa inayofanywa na Afisa wa Umma. | Mahakama ya Mkoa |
| 39 | Rushwa kwa Afisa wa Umma. | Mahakama ya Mkoa |
| 40 | Kuomba au kupokea faida kinyume na sheria kwa mtu anayefanya au kutekeleza maamuzi ya mahakama. | Mahakama ya Mkoa |
| 41 | Rushwa katika minada. | Mahakama ya Mkoa |
| 42 | Ushawishi wa siri katika kutoa ushauri. | Mahakama ya Mkoa |
| 43 | Rushwa kwa ajili ya kutoa msaada kuhusu mkataba. | Mahakama ya Mkoa |
| 44 | Kumdanganya mkuu. | Mahakama ya Mkoa |
| 45 | Mgongano wa maslahi. | Mahakama ya Mkoa |
| 46 | Faida isiyoruhusiwa kwa wadhamini kwa kuteuliwa. | Mahakama ya Mkoa |
| 47 | Rushwa ya zabuni. | Mahakama ya Mkoa |
| 48 | Matumizi mabaya ya wadhifa. | Mahakama ya Mkoa |
| 49 | Uhaulishaji wa mapato ya rushwa. | Mahakama ya Mkoa |
| 50 | Rushwa katika uchaguzi. | Mahakama ya Mkoa |
| 51 | Rushwa ya Afisa wa kigeni. | Mahakama ya Mkoa |
| 52 | Kushawishi au kutoa rushwa ya ngono. | Mahakama ya Mkoa |

## C. MAKOSA MENGINE

| KIFUNGU | KOSA | MAHAKAMA |
|---|---|---|
| 5 | Kushindwa kutekeleza maagizo ya Mamlaka. | Mahakama ya Wilaya |
| 7 | Kutotii amri halali ya Mkurugenzi Mkuu. | Mahakama ya Wilaya |
| 15 | Kutoa siri. | Mahakama ya Wilaya |
| 17 | Uzuiaji wa uchunguzi. | Mahakama ya Wilaya |
| 18 | Kushindwa kushirikiana na mchunguzi. | Mahakama ya Wilaya |
| 21 | Kushindwa kutekeleza amri ya Mamlaka. | Mahakama ya Wilaya |
| 24 | Kushindwa kuwasilisha taarifa inayohusiana na mali za mtuhumiwa. | Mahakama ya Wilaya |
| 25 | Kushindwa kuwasilisha taarifa za mali za mshirika wa mtuhumiwa. | Mahakama ya Wilaya |
| 27 | Kushindwa kutoa taarifa ya kumbukumbu na mali. | Mahakama ya Wilaya |
| 32 | Utoaji wa taarifa ambazo zinaweza kuharibu uchunguzi. | Mahakama ya Wilaya |
| 33 | Kujifananisha. | Mahakama ya Wilaya |
| 75 | Kushindwa kutekeleza Amri ya kuzuia mali inayotuhumiwa. | Mahakama ya Wilaya |
| 84 | Uvunjaji utamaduni na kanuni kuhusiana na mshirika wa kosa. | Mahakama ya Wilaya |
| 92 | Kumsaidia mtu kutenda kosa. | Mahakama ya Wilaya |
| 99 | Uonevu wa shahidi. | Mahakama ya Wilaya |
| 100 | Kushindwa kuripoti faida. | Mahakama ya Wilaya |

**IMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 23 Juni, 2023.

…………………………………………

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***